
# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 10 | Novemba 6, 2022 JARIDA LA JUMAPILI BILA MALIPO

# FUNDI WA UCHUMI WA RUTO

**David Ndii, mwanauchumi mbishani aliyepata umaarufu wakati wa aliyekuwa Rais Mwai Kibaki, anaongoza shughuli zote Ikulu kwa injili yake ya mfumo wa kiuchumi wa Bottom-Up**

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

# anywhere, anytime.

Follow the link to subscribe

> *epaper.nation.africa.*

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play




Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111

Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

## Yaliyomo

**5 KINOTI, HAJI NA MIZIMU YA ICC:** Je, DPP akifuatilia kesi kuhusu dhuluma zilizotekelezwa na polisi katika uchaguzi wa 2017 chini ya mwongozo wa uhalifu wa kimataifa wa uwajibikaji wa mamlaka, wavu wake utamfikia rais?

**10 SHIDA YA IMF YAZIDI:** Serikali mpya ya Rais Ruto imejipata katika hali isiyoweza kuepuka kutokana na mpango wa miezi 38 wa shirika hilo uliokitwa katika masharti magumu yanayohitaji mageuzi yasiyo maarufu ya kisiasa katika sekta kadhaa.

**18 UHAMASISHAJI WA AFYA YA AKILI:** Dkt Dorcas Magai amejitolea kuhakikisha kuwaWakenya wote wanapata huduma za kisaikolojia.

**22 KENYA TAYARI KWA DUNIA:** Waziri wa Kigeni na Masuala ya Ughaibuni Alfred Mutua anaelezea sera ya kigeni ya serikali ya Ruto, inayoweka mbele utafutaji wa masoko barani Afrika na kwingine.



# Katika minyororo ya IMF: Nidhamu ya hali ya juu itahitajika kuokoa uchumi

Serikali ya Rais William Ruto iko katika hali isiyoepukika nzuri kuhusu uchumi.

Madeni ambayo yamerundikana kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita yanameza mapato yanayotokana na ushuru, na ni vigumu pesa kubaki kugharama idadi kubwa ya watumishi wa umma na kulipia majukumu mengine ya serikali kama vile usalama, afya na elimu.

Gharama ya maisha imepanda kupita kiasi, kutokana na kiangazi kikali kinachoshuhudiwa nchini na vita kati ya Urusi na Ukraine vilivyochangia kupanda kwa bei ya chakula kiasi kwamba familia nyingi haziwezi kuimudu.

Bei ya mafuta inapanda kila mara, ikisambaza mfumko wa bei katika sekta zote za uchumi kupitia kupanda kwa gharama ya uchukuzi, inayochangia kupanda kwa bei za bidhaa na huduma zote.

Thamani ya shilingi ya Kenya inashuka kila mara, hivyo kufanya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje kuwa ghali na pia kuongezea gharama ya madeni yetu.

Wakati huo huo, wananchi wana matumaini makubwa kutokana na ahadi ambazo vigogo wa Kenya Kwanza walitoa wakati wa kampeni. Itakuwa vigumu kurudisha uchumi katika hali yake ya zamani na kutimiza ahadi nyingi za kampeni.

Sawa na kuongeza chumvi kwenye kidonda, ujumbe wa Shirika la Kifedha Ulimwenguni (IMF) uko nchini kufuatilia jinsi serikali inazingatia masharti iliyoweka ilipoipa mkopo ambao ungetolewa kwa kipindi cha miezi 38.

Shirika hilo lilihitaji serikali kutekeleza mageuzi machungu kisiasa, katika sekta kadhaa.



**Washington Gikunju**

**Shirika la IMF linaitaka Kenya Power iongeze bei ya stima ili kufidia hasara ya Sh26.3 bilioni kwenye rekodi zake za kifedha, hatua ambayo huenda ikapingwa na Wakenya wengi ambao tayari wanalipa mojawapo ya bei za juu zaidi za stima barani Afrika.**

Mnamo Aprili 2021, IMF iliidhinisha mkopo wa dola 2.3 bilioni (Sh250 bilioni) kwa Kenya ambao uliambatanishwa na masharti magumu. Baadhi ya masharti hayo ni kuimarishwa kwa usimamizi wa mikopo.

Shirika hilo la kifedha linataka viwango vya madeni vipunguzwe, kuzimwa kwa udhamini wa mikopo kwa serikali za kaunti na mashirika ya serikali na kudhibitiwa kwa hamu ya kuchukua mikopo mipya kutoka nje.

IMF iliyo na makao yake makuu jijini Washington, Amerika, inaitaka Kenya Power iongeze bei ya stima ili kufidia hasara ya Sh26.3 bilioni kwenye rekodi zake za kifedha, hatua ambayo huenda ikapingwa na Wakenya wengi ambao tayari wanalipa mojawapo ya bei za juu zaidi za stima Afrika.

Aidha, IMF inataka kupanuliwa kwa mawanda ya ulipaji ushuru, kuondolewa kwa ruzuku kwa bei ya mafuta, mageuzi katika shirika la ndege, Kenya Airways, kuchapishwa kwa ripoti ya ukaguzi kuhusu matumizi ya fedha za Covid-19, kuchapishwa kwa wamiliki wa kampuni ambazo hupewa kandarasi za umma na mabadiliko katika sheria ya kudhibiti ulanguzi wa fedha.

Serikali ya Ruto ina chaguo dogo, kwa muda mfupi na pengine kwa muda wa kati, isipokuwa kutiii masharti hayo ama kushauriana na IMF kwa kunyenyekea ili baadhi ya masharti yalegezwe.

Itabidi serikali iweke nidhamu katika matumizi ya fedha au sera bunifu za kiuchumi kufikia uhuru kiuchumi ambao utawala wa Hayati Rais Mwai Kibaki ulirithisha taifa hili.

Ni ufufuzi halisi wa kiuchumi pekee ambao utasaidia serikali ya Ruto kujikomboa kutoka katika pingu za IMF iwapo inataka uhuru wa kutekeleza sera zake za kiuchumi.

Kama asasi nyingi ya kukopesha, IMF huweka mashartu magumu kwa mikopo yake ili kupata hakikisho la ulipaji. Lakini hailengi kuinasua Kenya kutoka na changamoto za kiuchumi zinazoizonga sasa.

Lakini serikali isisahau kuwa inawajibika kwa wapigakura. Ni lazima ichague kwa hekima masharti ya IMF ambayo itatekeleza, lakini pia itafute namna ya kusaidia masikini kwa kuepuka kuongeza ushuru, kufuta watu kazi na hatua zingine zinazoweza kupandisha gharama ya maisha.

*wgikunju@ke.nationmedia.com*

*- Zimetafsiriwa na Charles Wasonga*

Darubini Ya Wiki

Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Mutuma Mathiu** Mhariri Mkuu

**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji

**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ 27 wapendekezwa kwa nafasi 9 za EALA

# Wabunge kuhoji IG mteule Koome

Kikao cha pamoja cha Kamati ya Bunge Jumanne, wiki ijayo kitampiga msasa Inspekta Jenerali wa Polisi mteule Japhet Koome. Hatua hii inafuatia kukamilika kwa muda wa mawasilisho ya umma Alhamisi wiki iliyopita. Baada ya kikao cha Jumanne, kamati ya pamoja - Kamati ya Bunge la Kitaifa kuhusu Usimamizi na Masuala ya Nchi na Kamati ya Seneti inayosimamia Usalama wa Kitaifa, Ulinzi na Mahusiano ya Kigeni – itachukua likizo ya kuandika ripoti, ambayo itawasilishwa mbele ya Bunge ambalo litamuidhinisha ama kumkataa mteule.
Rais William Ruto alituma jina la Koome kwa Bunge katikati mwa Oktoba. Kamati ya pamoja ya Bunge pia inatarajiwa kuanza kuwapiga msasa waliopendekezwa kwa Bunge la Afrika Mashariki kujaza nyadhifa tisa zitakazogawanywa baina ya vyama vya kisiasa. Jopokazi hilo la wanakamati 14 litatathmini majina 27 yaliyopendekezwa kwa kamati na vyama mbalimbali vya kisiasa kati ya Novemba 10 na 11. Kisha kura itapigwa katika Seneti na Bunge la Kitaifa kupunguza idadi hiyo had majina tisa yatakayowakilisha Kenya katika bunge hilo la kanda. Ni Kenya na DRC pekee ambazo hazijawasilisha majina ya wawakilishi wake.



Kikao cha Bunge la Kitaifa mnamo Oktoba 6.

■ Familia: Hawezi kudhibiti maisha yake

# Tiba kwa 'Britney Spears' wa Misri



Katika wiki chache zilizopita, kisa cha mwanamuziki nyota wa Misri aliyelazwa katika kituo cha kubadilisha tabia kiliibua mjadala mpya kuhusu haki za wanawake katika taifa hilo lenye itikadi kali. Sherine Abdel Wahab kwa miaka mingi amependa muziki wa kisasa wa Kiarabu, lakini matukio ya hivi majuzi yamempa jina 'Britney Spears wa Misri'- si kutokana na talanta yake ya muziki bali kutokana na juhudi za familia yake za kumuonyesha kuwa asiyeweza kujisimamia kimaisha. Mashabiki wake walishangaa alipolazwa katika kituo cha kurekebisha tabia mwezi uliopita hatua iliyoibua mjadala mkali.

■ UN: Ungeni mkono 'hatua hiyo ya kijasiri'



Aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta, Redwan Hussein, Mwakilishi wa serikali ya Ethiopia (wa pili kushoto), balozi wa Umoja wa Afrika katika Upembe wa Afrika ambaye pia alikuwa Rais wa Nigeria, Olusegun Obasanjo (wa pili kulia) na Getachew Reda, Mwakilishi wa kundi la wapiganaji la Tigray People's Liberation Front (TPLF), wakishuhudia kutiwa sahihi kwa mkataba wa amani jijini Pretoria mnamo Novemba 2. PICHA | AFP

# Viongozi wapongeza amani Ethiopia

Viongozi duniani wamepongeza mkataba uliotiwa sahihi na pande husika katika mapigano ya Ethiopia kumaliza mzozo huo wa miaka miwili. Mkata huo ulitiwa saini Jumatano nchini Afrika Kusini na kusimamiwa na Umoja wa Afrika (AU). Rais wa Senegal na mwenyekiti wa sasa wa AU, Macky Sall, walitaja tangazo hilo kuwa "habari njema". Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres, amepongeza mkataba huo na kuhimiza raia wote wa Ethiopia na jamii ya kimataifa kuunga mkono "hatua hiyo ya kijasiri" iliyochukuliwa na pande hizo mbili hasimu. "Mkataba huo ni hatua ya kwanza muhimu katika kumaliza mzozo huo mbaya wa miaka miwili ambao umeangamiza maisha ya maelfu ya raia wa Ethiopia," akasema. Waziri wa Mashauri ya Kigeni Amerika, Antony Blinken, alipongeza hatua hiyo akisema nchi yake itaunga mkono juhudi zinazoongozwa na AU katika wiki zijazo. Rais wa Kenya William Ruto, Waziri wa Mashauri ya Kigeni Ujerumani, Annalena Baerbock na Umoja wa Nchi za Ulaya, wote walipongeza juhudi za kurudisha amani Ethiopia. Lakini wapatanishi wameonya bado kuna kazi ya kufanya. "Suluhisho la kudumu linapatikana tu kupitia ushirikiano wa kisiasa na kukubali tofauti zetuhuku tukibakia Ethiopia iliyoungana," akasema aliyekuwa rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, aliyesaidia kufanikisha mkataba huo.

■ Ataigiza pamoja na nyota wa Bollywood Priyan-

# Céline Dion kujiigiza katika rom-com



Mwanamuziki maarufu Celine Dion ataigiza katika filamu ya mapenzi na ucheshi kwa jina 'Love again', itakayozinduliwa kwenye vituo vya maigizo baadaye 2023 - ambapo ataigiza nafsi yake. "Tuonane kwenye filamu!" akaandika kwenye mitandao yake ya kijamii, akisema ataigiza pamoja na mwigizaji mashuhuri wa filamu za Kihindi za Bollywood, Priyanka Chopra Jonas na mwigizaji nyota wa Scotland Sam Heughan, maaurufu kwa uigizaji wake katika sinema ya 'Outlander'. Filamu hiyo iliyobuniwa na kampuni ya Sony, itazinduliwa rasmi Mei 12. Inasimulia hadithi ya msichana anayeendelea kumtumia jumbe za simu mchumba wake baada ya kifo chake. Mapenzi yanachipuka kati yake na mmiliki mpya wa nambari hiyo ya simu.

*- Zimetafsiriwa na Mary Wangari*


ePaper Copy Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ DHANA YA UWAJIBIKAJI KATIKA MAMLAKA

# KINOTI, HAJI NA MAPEPO YA ICC

*DPP ameapa kufungua upya kesi ya mauaji ya mtoto Pendo na vitendo vingine vya ghasia za polisi wakati wa uchaguzi mkuu wa 2017 chini ya uhalifu wa kimataifa na uwajibikaji katika mamlaka. Je, anaweza kufanya hivyo hata kwa Rais?*



Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma Noordin Haji

● Na MACHARIA GAITHO

Inaonekana mambo yameanza kuharibika kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Uhalifu George Kinoti, lakini mtego huo unaweza kupanuka na kupanda juu zaidi huku Rais William Ruto akishinikiza uchunguzi kuhusu mauaji ya kiholela na uhalifu mwingine unaodaiwa kutekelezwa chini ya utawala wa mtangulizi wake, Rais Uhuru Kenyatta.

Kwa sasa jambo linaloangaziwa ni kutekwa nyara na kushukiwa kuuawa kwa raia wawili wa India, Mohammed Said Sami na Zulfiqar Ahmed, ambao walikuwa wamesajiliwa na kundi la kampeni la Ruto na dereva wao Mkenya, Nicodemus Mwanzia, ambapo maafisa tisa kutoka kitengo kilichovunjwa cha DCI cha Special Services Unit (SSU) wamekamatwa.

Katika kesi ya aina hiyo, kuna uwezekano kuwa baadhi ya washukiwa tayari wamekubaliana na wachunguzi. Kulingana na duru zinazofahamu hali ya uchunguzi zilizozungumza na Darubini ya Wiki, juhudi zinaendelea za kushawishi baadhi ya waliokamatwa kumwaga mtama kuhusu kilichotendeka na aliyewapa amri, na pia kutoa ushahidi dhidi ya wenzao na wakubwa wao ili wao wasichukuliwe hatua kali.

Kinoti pia yuko katika presha baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma Noordin Haji kuondoa kesi nyingi za ufisadi na aina nyingine za uhalifu dhidi ya washirika wa Ruto, akiwemo Naibu Rais Rigathi Gachagua, akimlaumu mkuu huyo wa zamani wa DCI kwa kuwasilisha kortini ushahidi wa uongo.

Jumapili iliyopita, Haji alitangaza kwenye mahojiano na KTN kuwa Kinoti atashtakiwa ikigunduliwa alighushi ushahidi dhidi ya Gachagua, akidai kuwa DCI alimsukuma kumshtaki Naibu Rais kwa kutegemea ushahidi ambao sasa imebainika ulikuwa wa uongo.

Haya yalijiri baada ya maafisa kadhaa waliochunguza kesi hiyo kuwasilisha hati mpya za kiapo wakidai walilazimishwa na Kinoti kubuni ushahidi dhidi ya aliyekuwa wakati huo Mbunge wa Mathira.

Hata hivyo, nia ya serikali hasa ilielezewa na tangazo la Haji siku mbili zilizotangulia kuwa kesi ya mauaji ya mtoto Pendo na vitendo vingine vya ghasia za polisi wakati wa uchaguzi mkuu wa 2017 zitafunguliwa upya chini ya mwongozo wa kesi za uhalifu wa kimataifa kuhusu uwajibikiaji wa amri.

Huu ndio msingi ambao, katika mauaji ya halaiki, uhalifu dhidi ya binadamu, kutimua watu makwao, mateso na uhalifu wa kingono wakati wa vita, uwajibikaji huwa si kwa wanaoutekeleza hasa, bali kwa wakubwa wao, wanaoupanga, wafadhili na hata juu zaidi wanaochukuliwa kuwajibika kisiasa. Huchukuliwa kuwa wenye hatia hata kama hawakuwa karibu na eneo la uhalifu.

Haji alidokeza kuwa vibali vimetolewa kuwakamata maafisa wakuu wa polisi ndani ya eneo lililoathiriwa ukanda wa Nyanza - wakiwemo makamanda wa vituo, tarafa, kaunti na ukanda.

Lakini dhana ya kuwajibika kwa wakuu au makamanda pia inamaanisha kuwa mtego huo unaweza kupanuliwa kwa upana na kwenda juu.

Chini ya msingi huu, yanaweza kwenda zaidi ya makamanda wa nyanjani kujumuisha Mkurugenzi wa DCI, Manaibu Inspekta Jenerali wa Huduma ya Polisi Kenya na Polisi Tawala, Inspekta Jenerali wa Polisi na maafisa wengine wakuu ambao huenda walihusika kupanga na kutekeleza uhalifu unaochunguzwa.

Wengine walio katika orodha hiyo chini ya mwongozo wa ICC wanaweza kuwa wakuu wa kiraia wanaowajibikia usimamizi wa idara za usalama, wakiwemo Waziri na Katibu wa wizara ya Usalama wa Ndani, Idara ya Serikali inayohusika na polisi.

Hatimaye, hii inaweza kumhusisha Rais mwenyewe kwa kudhaniwa alinufaika na ghasia zozote zilizotekelezwa na polisi kwa raia. Hata hivyo, Kinoti hakuwa katika ofisi wakati uhalifu unaodaiwa ulipotekelezwa katikati ya Agosti 2017. Aliteuliwa na Rais Kenyatta wiki ya kwanza ya Januari 2018, kumrithi Bw Ndegwa Muhoro, aliyeteuliwa Balozi wa Kenya nchini Malaysia.

Inspekta Jenerali wa polisi Hillary Mutyambai ambaye, sawa na Kinoti, aliondoka katika huduma ya polisi Rais Ruto alipoingia mamlakani Septemba, hakuwa ofisini wakati huo. Aliteuliwa Aprili 2019 kumrithi Joseph Boinett ambaye walihudumu pamoja kama maafisa wa Huduma ya Taifa ya Ujasusi.

Manaibu wawili wa Boinett walikuwa Bw Joel Kitili (Kenya Polisi) na Samuel Arachi (Polisi Tawala) ambao wote wameondoka ofisini.

Katika taarifa iliyotolewa Oktoba 28, Haji alisema uchunguzi unaoendelea wa mauaji ya mtoto Samantha Pendo mnamo Agosti 8, 2017, ambayo yalilaaniwa kitaifa, ulifichua ghasia za polisi zilizopangwa, ambazo, kwa mara ya kwanza katika historia ya Kenya, zilihitaji kuchukuliwa kama mashtaka ya uhalifu dhidi ya binadamu chini ya sheria za Kenya kwa kutumia Sheria ya Uhalifu wa Kimataifa.

Haji alifichua kuwa ghasia dhidi ya raia katika mitaa ya Nyalenda, Nyamasaria, Kondele na Obunga mjini Kisumu zilitekelezwa chini ya operesheni ya polisi iliyofahamika kama 'Mipango ya Baada ya Uchaguzi', ikiwa na mfumo wa amri uliojumuisha wakuu wa vitengo na makamanda wa sekta tofauti.

Ilibainika kuwa ghasia hizi, hazikulipuka tu, lakini zilipangwa na kushirikishwa na maafisa wa vyeo vya juu ambao majina yao hayakufichuliwa ambao wanaweza kushtakiwa kwa makosa ya mauaji, ubakaji na mateso kama uhalifu dhidi

Endelea Uk 6

Nation Media Group "ePaper Copy"

kurunzi ya kenya

# Wasiwasi kuhusu ‘uwajibikaji katika mamlaka’



Rais William Ruto



Aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta



Aliyekuwa Waziri wa Usalama wa Ndani Fred Matian



Aliyekuwa Mkuu wa Polisi Mohammed Hussein Ali



Mwanahabari wa radio Joshua Sang

Kutoka Uk 5

ya binadamu. Hatua ya DPP ya kutofichua majina ya maafisa watakaoshtakiwa inalingana na mtindo wa ICC ambapo mashtaka yanaweza kuwasilishwa kortini na vibali vya kukamata washukiwa kutolewa kabla yao kukamatwa.

Hata hivyo, hakufichua iwapo tayari ametumia mtindo huo wa kwenda kortini au iwapo kuna wale ambao wamekamatwa.

Kilicho muhimu ni kuwa hakuna asiyeweza kushtakiwa chini ya mfumo wa ICC kwa kuhusika na uhalifu. Pengine haikutokea tu, kuwa, baada ya taarifa ya Haji, mwanapropaganda mkuu wa Rais Ruto katika mitandao ya kijamii, Dennis Itumbi, aliandika kwenye Twitter maneno ya dharau anayotumia kumaanisha aliyekuwa Waziri wa Usalama wa Ndani Fred Matiang’i.

Hakusema alichomaanisha kwa kutaja Matiang’i, lakini wakati wake kufanya hivyo unaashiria kinachojiri. Darubini ya Wiki ilimpigia simu Matiang’i kupata kauli yake, lakini hakujibu simu zetu.

Ni muhimu kufahamu kuwa Haji anapendekeza kutumia dhana sawa ya kuwajibikia mamlaka ambayo ICC ilitumia kushtaki Uhuru na Ruto kuhusiana na ghasia za baada ya uchaguzi mkuu wa 2007 ambapo watu zaidi ya 1,200 walipoteza maisha yao na zaidi ya 600,000 wakatimuliwa makwao.

Wengine walioshtakiwa kwa kuwajibikia mamlaka ni aliyekuwa Mkuu wa Utumishi wa Umma Francis Muthaura, aliyekuwa Kamishna wa Polisi Mohammed Hussein Ali na aliyekuwa Waziri Henry Kosgey. Mshtakiwa wa sita alikuwa mtangazaji wa kituo cha redio cha Kass FM, Joshua Sang.

Wote sita walishtakiwa sababu tofauti baada ya uchunguzi kukamilika, lakini kesi za ICC zilitoa funzo moja kubwa: kwamba hakuna njia ya wanaopanga na kutekeleza ghasia kukwepa uwajibikaji.

Hasa, mpinzani aliyeshindwa na Ruto katika uchaguzi mkuu wa 2022, Raila Odinga, alitaja kesi za ICC kuwa sababu iliyomfanya asiitishe maandamano ya umma kulalamikia matokeo ya uchaguzi na kutupwa kwa kesi yake na Mahakama ya Upeo.

Hata hivyo, mipango ya DPP ya kuwashtaki wakuu wa polisi na mashtaka ya kuwajibikia mamlaka ni hali tete ambayo imefanya baadhi ya washirika wa Ruto kmuonya awe mwangalifu.

Sababu moja ni kwamba mrithi wa Kinoti katika DCI, Mohammed Amin, Kaimu Inspekta Jenerali, Noor Gabow, na maafisa wengine wengi ambao walishikilia nyadhifa kuu katika muundo wa amri wa polisi mnamo 2017 wanaweza kuhusishwa.

Hata kigumu zaidi ni kuwa, iwapo hatimaye Uhuru ndiye alinufaika na ghasia za polisi Kisumu, mgombea mwenza wake, Ruto, alinufaika pia.

Na pia akiwa Naibu Rais na mwanachama wa Baraza la Kitaifa la Usalama, inawezekana Ruto alifahamu maamuzi yote katika kiwango hicho.

Kisha kuna ukweli kuwa mashtaka, yawe kuhusu ghasia za polisi Kisumu mwaka wa 2017 au mauaji ya kiholela yaliyohusishwa na kitengo cha SSU cha DCI wakati wa muhula wa Kinoti hayakutekelezwa na maafisa “wahalifu” jinsi inavyoripotiwa.

Katika kesi nyingi, operesheni za vitengo kadhaa spesheli huamrishwa katika viwango vya juu vya polisi, na pia na maafisa wa kiraia katika kiwango cha mawaziri, Baraza la Kitaifa la Usalama na Kamati ya Ushauri ya Usalama wa Kitaifa.

Vitengo kama cha Polisi wa kukabiliana na Ugaidi na vingine vinavyopigana na uhalifu ikiwemo SSU na watangulizi wake kama Special Crime Prevention Unit, Flying Squad na vingine, huwa vinapokea amri kutoka viwango vya juu serikalini kuzuia vitisho vibaya kwa usalama wa taifa kama genge la wahalifu wa Mungiki eneo la Kati mwa Kenya, sehemu za Rift Valley na Nairobi, magaidi wa al Shabbab katika maeneo ya Pwani na Kaskazini Mashariki na February Eighteenth Freedom Army (Fera) katika kaunti za Bungoma na Trans Nzoia.



Aliyekuwa Mkuu wa DCI George Kinoti

Kabla ya kuteuliwa DPP mnamo Machi 2018, Haji alikuwa amehudumu kwa muda mrefu kama afisa wa cheo cha juu katika Huduma ya Taifa ya Ujasusi, ambapo bila shaka alipata tajiriba pana katika operesheni zinazohusisha idara tofauti kwa lengo la kuangamiza muundo wa al-Shabbab, usajili na mafunzo ya itikadi kali kote Kenya.

Waathiriwa wanajitokeza sana katika orodha ya visa vya mauaji ya kiholela vinavyochunguzwa na Mamlaka Huru ya Kuchunguza Utendakazi wa Polisi na mashirika kadhaa ya kutetea haki za binadamu inayotolewa sasa baada ya uongozi mpya Ikulu.

Changamoto nyingine kwa Haji ni kuwa atakuwa na wakati mgumu kueleza wakati wake wa kuondoa kesi za uhalifu zilizohusisha washirika wa Ruto na vitisho vya kushtaki Kinoti kwa ushahidi wa uongo, na pia kufungua upya kesi za ghasia za uchaguzi mkuu wa 2017. Darubini ya Wiki ilipiga simu katika Afisi ya Haji kupata kauli zake. Afisa wa mawasiliano aliahidi kutupigia simu, lakini hakuwa amefanya hivyo wakati wa kwenda mitamboni.

Kwa Haji kukiri kuwa alifungua kesi za uhalifu kwa kutumia ushahidi wa uongo chini ya shinikizo za kuridhisha wanasiasa waliokuwa na ushawishi wakati huo ni sawa na kujilaumu ambako kunaweza kumfanya ashtakiwe pia na kuondolewa ofisini.

Vile vile, anatoa ishara kuwa, iwapo kiongozi mkuu wa mashtaka alikubali presha chini ya utawala wa Uhuru, anafanya hivyo chini ya utawala wa Ruto, na kutilia shaka uadilifu wa maamuzi anayofanya kwa kuondoa au kufungua mashtaka ya uhalifu.

Kuna uwezekano wa Haji kuwekewa presha zaidi siku zijazo ajiuzulu, huku makundi kadhaa ya kutetea haki za binadamu na ya kisheria yakimlaumu kwa kusaliti kiapo cha ofisi yake.

Ofisi ya DPP kisheria, inafaa kuwa huru na kukingwa dhidio ya presha na maagizo kutoka kwa idara yoyote, lakini sasa anaonekana kufuata maagizo ya serikali ya Ruto.

*-Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA YA UMMA

# MAMBO NI SHWARI LICHA YA DHORUBA

*Akionekana kutobabaishwa na dhoruba aliyosababisha kwa kuondoa kesi kubwa za uhalifu, huenda Haji haelewi hatari ya kupuuza malalamishi kuhusu wakati wake wa kuondoa kesi hizo, au ana imani kubwa kuhusu uamuzi wake*

● NA MACHARIA GAITHO

Kwa mtu aliyejipata katikati ya dhoruba ya shutuma za umma kuhusu uamuzi wake tata wa kuondoa kesi za uhalifu dhidi ya washirika wakuu wa Rais William Ruto punde tu baada ya mabadiliko ya uongozi katika Ikulu, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP) Noordin Haji anaonekana mtulivu na asiye na wasiwasi.

Akiandamana na kundi la waendesha mashtaka wa vyeo vya juu wanaosimamia idara tofauti, Haji anapokea Darubini ya Wiki katika ukumbi wake wa mikutano akionekana kutojali kimbuga alichoachilia ambacho kimechochea miito ya kumtaka ajiuzulu kutokana na madai kwamba anabadilisha ofisi hiyo huru kuwa chombo cha kutumiwa na serikali mpya.

Kwa kutegemea jinsi mtu anavyoitazama, anaweza kuwa haelewi kabisa ya kupuuza malalamishi kuhusu wakati wake wa kuondoa kesi hizo au ana imani kubwa kuhusu maamuzi yake licha ya mtikisiko wa kisiasa ambao yamezua.

Muungano wa Ruto wa Kenya Kwanza ulikita kampeni yake kwa kauli mbiu 'Uhuru Unakuja'.

Kuondolewa kwa kesi za uhalifu dhidi ya Mawaziri Aisha Jumwa na Mithika Linturi, aliyekuwa Afisa Mkuu Mtendaji wa Kenya Power Ben Chumo na wengine, na pia ishara ya kuporomoka kwa kesi ya ufisadi dhidi ya Naibu Rais Rigathi Gachagua, kulichochea vichwa "Uhuru Umekuja' katika vyombo vya habari.

Hasa, wakati wa kampeni, Gachagua alijigamba wazi kuwa kesi inayomkabili ingeondolewa punde tu Ruto akiwa rais. Wakati msururu huu wa matukio unapobainishwa kwa Haji, anaonekana kutojali, akieleza historia ya kila kesi kwa subira na sababu ya kuondolewa.

Pia, kuna ufichuzi wake Jumapili iliyopita kwamba alisukumwa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Uhalifu George Kinoti kufungua mashtaka kwa kutegemea ushahidi wa uongo, kigezo ambacho kinaweza kumfanya Haji kuwa na makosa katika maovu yanayodaiwa.

Lakini kulingana naye, afisi yake haijawahi kushtaki mtu yeyote ikijua ushahidi ulikuwa wa uongo.

Kilichofanyika ni kuwa kitendo hicho kilijulikana baadaye katika hati ya kiapo ya afisa aliyechunguza kesi ya Gachagua ambaye alidai aliwekewa presha na Kinoti. Kesi hiyo itaporomoka tu ingawa haikuwa imeondolewa rasmi wakati wa kuandika habari hii.

Kuhusu kesi ya Aisha Jumwa, mashtaka yalifunguliwa baada ya wachunguzi wa DCI kuwasilisha ushahidi ambao ulitimiza viwango vya kufungua mashtaka, lakini walikataa kutimiza ahadi ya kujaza mapengo yaliyotambuliwa na ODPP.

Kuna mawasiliano ya barua yaliyoanza 2019 huku upande wa mashtaka ukisukuma DCI kuwasilisha ushahidi bila mafanikio. Hali ilikuwa sawa katika kesi dhidi ya Chumo na wakuu wengine wa Kenya Power.

Katika kesi ya jaribio la ubakaji iliyomkabili Linturi, ilikuwa suala la mwathiriwa kuondoa malalamishi yake na si upande wa mashtaka ulioondoa kesi.

Kulingana na Haji, upande wa mashtaka unakubali kwa nia njema habari, ushahidi na eksibiti zinazowasilishwa na wachunguzi. Wanachunguza ushahidi na kupima iwapo unatimiza vigezo vya kufungua mashtaka. Mara kwa mara, wachunguzi huwa wanaelekezwa maeneo yanayohitaji uchunguzi zaidi.

Wakati mwingine, mashtaka huanza uchunguzi ukiendelea, mradi tu imeamuliwa kwamba kesi inaweza kufaulu katika korti ya sheria mapengo yaliyotambuliwa yakijazwa.

Kama ni kweli Kinoti na maafisa wake walitumia ushahidi wa uongo, je watakamatwa na kushtakiwa? Kuhusu hilo, Haji hana hakika, akisema tu kwamba suala hilo linachunguzwa na ni wakati awamu hiyo itakamilika ambapo uamuzi utafanywa.

Hata hivyo, anaongeza, mashtaka yanayoweza kutokana na uchunguzi huo, yatashughulikiwa na waendeshaji huru wa mashtaka kuepuka mgongano wa maslahi.

Kisha kuna suala la kuvunjwa kwa kitengo cha Special Service Unit cha DCI na uchunguzi kuhusu mauaji ya kiholela, na pia mashtaka kutokana na mauaji ya polisi Kisumu kufuatia uchaguzi mkuu wa 2017.

Haji anakataa katakata kwamba hatua hiyo ina ushawishi wa kisiasa kufuatia kuingia mamlakani kwa Ruto, akisisitiza kuwa kila kesi inachukuliwa kivyake na muda wa kuamua kufungua mashtaka hauna chochote kuhusu siasa lakini unatokana na kukamilika kwa uchunguzi mgumu, baadhi uliochukua zaidi ya miaka mitano.

Inaweza pia kuwa ni sadfa lakini ukweli ni kwamba, baada ya masuala haya kuibuka punde tu baada ya Rais Ruto kuingia mamlakani, itakuwa vigumu kushawishi walio na shaka kwamba hakuna uhusiano.

Ingawa huenda Haji hana uwezo kuhusu haya, si siri kwamba baadhi ya washirika wa karibu wa Ruto wanatamani kutumia nguvu mpya walizopata na kudhibiti idara muhimu za polisi kufanya maisha kuwa magumu kwa maadui wao katika muundo wa mamlaka wa rais aliyeondoka Uhuru.

Katika mashtaka yanayosubiriwa ya makamanda wakuu wa polisi katika kesi ya Mtoto Pendo chini ya mwongozo wa Uhalifu wa Kimataifa, watakaofikishwa kortini walihusika moja kwa moja na eneo la operesheni, lakini dhana ya kuwajibikia amri inayotumiwa inaweza kufungua milango ya kupanua uchunguzi hadi makao makuu ya polisi jijini Nairobi na hata viongozi wa kisiasa.

Hali kwamba viongozi wapya wa polisi wamekuwa wakipokea maagizo moja kwa moja kutoka kwa Ruto kuhusu jinsi ya kuendesha baadhi ya uchunguzi inaweza kuwanyima usingizi baadhi ya maadui wake.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*



Mkurugenzi wa Mashataka ya Umma Noordin Haji


ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ BARAZA LENYE NGUVU LA WASHAURI WA KIUCHUMI

# WATAALAMU WAKUU WA RAIS

*Ndii anaongoza kundi la watalaamu wa kiuchumi ambao wamepewa uhuru wa kuunda sera na kufanya mageuzi. Sawa na Afisi ya Usimamizi wa Bajeti katika Ikulu ya White House, wataalamu hao wanahudumu kutoka Ikulu na humfikia Rais bila vikwazo*



**David Ndii, mwenyekiti wa Baraza la Rais la Washauri wa Kiuchumi.** PICHA | SILA KIPLAGAT

• Na JAINDI KISERO

Ilitarajiwa kuwa Rais William Ruto angemteua mwanauchumi maarufu, na msomi, Dkt David Ndii katika wadhifa mkuu katika sekta ya uchumi, kama vile Hazina ya Kitaifa.

Habari kwamba Ndii aliteuliwa mwenyekiti wa Baraza la Washauri wa Kiuchumi wa Rais ilishangaza hasa kwa sababu wadadisi wa sera za kiuchumi hawakuelewa mchango wa asasi hiyo mpya katika kuathiri sera za serikali ikilinganishwa na mamlaka ya Hazina ya Kitaifa na Benki Kuu ya Kenya (CBK).

Je, asasi hii ingekuwa sawa na Baraza la Kitaifa la Kiuchumi (NESC) - asasi iliyoongoza utayarishaji wa sera ya kiuchumi wakati wa utawala wa Rais wa zamani Mwai Kibaki, na iliyobuni Ruwaza ya 2030?

Hata hivyo, huenda wanaofuatilia uundaji wa sera ya kiuchumi chini ya utawala huu mpya wameng'amua kiwango cha ushawishi wa Ndii na kundi la wataalamu walioteuliwa juzi.

Darubini ya Wiki imepata habari kwamba Ndii na kundi lake wamehusika kwa kiwango kikubwa katika maamuzi ya juzi kuhusu mageuzi ya kifedha katika Shirika la Ndege Nchini, Kenya Airways.

Wiki jana, kundi hilo liliwaagiza wasimamizi wa shirika hilo wafike mbele yake kulifahamisha kuhusu tishio la marubani kugoma. Aidha, kundi la Ndii lilitaka kujua matokeo ya hatua ambayo sharti itekelezwe chini ya mpango uliopendekezwa na Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF) ikiwemo kujadiliana na kampuni za kimataifa za kukodisha kupunguza gharama ya ukodishaji, upunguzaji wa wafanyakazi na gharama ya mafuta.

Inaarifiwa kuwa baraza hilo, lililobuniwa na rais, limekuwa na usemi katika mipango mipya ya serikali kuhusu masuala kama vile kupunguza bajeti kwa Sh300 bilioni, kuongeza kiwango cha ukusanyaji ushuru kwa kupanua mawanda ya ukusanyaji na hitaji la uwekaji akiba kwa watakaofaidi kutokana na hazina ya hasla.

Katika Hazina ya Kitaifa, inaarifiwa kuwa kundi la Ndii limeendesha majadiliano mapana na kupendekeza mabadiliko ya mwel-

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Baraza la Rais kuhusu Masuala ya Kiuchumi na Afisi ya Masuala ya Kifedha na Bajeti ni asasi zinazotumiwa na serikali kufanikisha mfumo wa urais

David Ndii



Aliyekuwa Naibu Rais William Ruto akiwa na mwanauchumi David Ndii, Wabunge Kimani Ichungwah (Kikuyu), Rigathi Gachagua (Mathira, sasa Naibu Rais) na John Kiarie (Dagoretti Kusini) baada ya mkutano wa kupanga kampeni Kaunti ya Narok, Mei 2. PICHA | DPPS

ekeo katika kitengo cha kuongoza ushirikiano kati ya sekta ya umma na kibinafsi katika utekelezaji miradi na Afisi ya Kusimamia Mikopo.

Kando na Ndii, ambaye ni mwenyekiti wa baraza hilo, wanachama wengine ni mwanabenki mashuhuri Mohammed Hassan na Dkt Nancy Laibuni wa taasisi ya Kiprra.

Kando na baraza hilo, Dkt Kamau Thugge, ambaye awali amehudumu katika Hazina ya Kitaifa kama Katibu wa Masuala ya Kiuchumi na Katibu wa Wizara, anashikilia cheo cha mshauri na Mkuu wa Afisi ya Masuala ya Fedha na Sera ya Bajeti.

Dkt Augustine Cheruiyot ni mshauri na mkuu wa sekritariati kuhusu mabadiliko ya kiuchumi.

Wiki jana, Ndii alijitokeza kufafanua majukumu mapya ya wataalamu, wanaofanya kazi kutoka Ikulu, na jinsi wanaweza kuelekeza usimamizi wa masuala ya kiuchumi nchini.

Kwenye ujumbe kupitia Twitter, Ndii alielezea kuwa tofauti na NESC chini ya Kibaki, baraza hilo ni asasi tekelezi sawa na iliyo nchini Amerika.

"Baraza la Rais kuhusu Masuala ya Kiuchumi na Afisi ya Masuala ya Kifedha na Bajeti ni asasi zinazotumiwa na serikali kufanikisha mfumo wa uongozi wa urais," akasema Ndii.

Ni wazi kuwa wazo hilo limekopwa kutoka Amerika ambayo ina Afisi ya Usimamizi wa Bajeti katika Ikulu, Hazina ya Kitaifa na Afisi ya Bajeti katika Bunge la Congress.

Kubuniwa kwa afisi ya usimamizi wa bajeti kunafaa, ikizingatiwa kuwa taifa limekumbatia mfumo wa utawala wa kirais chini ya Katiba ya 2010.

Sababu ni kwamba, chini ya mifumo ya urais, Rais husimamia utekelezaji wa sera za kiuchumi, huweka malengo kuhusu viwango na utekelezaji wa bajeti huku akiachia Hazina ya Kitaifa wajibu wa utekelezaji wa bajeti na usimamizi wa fedha za nchi.

Siku za mwanzo za utawala wa Rais Kenyatta, kulikuwa na wazo kuhusu kubuniwa kwa Afisi ya Usimamizi wa Bajeti katika Ikulu. Lakini wazo hilo lilitupiliwa mbali.

Hivi ndivyo taifa liliishia kuendesha mfumo wa utawala wa urais chini ya muundo wa usimamizi wa kifedha wa mfumo wa utawala wa ubunge.

Inasubiriwa kuonekana iwapo asasi mpya zilizobuniwa katika Ikulu zitachangia kuwepo kwa mzozo wa kimamlaka na kuingiliana kwa utendakazi.

Lakini kulingana na jinsi asasi hizo za Ikulu zitaweza kupata nguvu na ushawishi katika usimamizi wa kifedha, Kenya inaelekea katika mfumo ambapo Rais, kwa mfano, atakuwa akiipa Hazina ya Kitaifa malengo kuhusu upungufu wa bajeti huku akisubiri kutazama na kutathimini utendakazi kwa misingi ya malengo hayo.

Mfumo wa urais unamruhusu Kiongozi wa Taifa kusimamia ukadiriaji wa kiasi cha rasilimali kwa sababu yeye ndiye hutoa ahadi nyakati za uchaguzi na anabeba mamlaka kutoka kwa wananchi.

Ikiwa utekelezaji wa mpango huu mpya utaanza, Hazina ya Kitaifa itaachiwa wajibu wa kukusanya ushuru, kukopa pesa na kusimamia fedha.

Kenya ilipopitisha Katiba ya 2010, wafuatiliaji wa usimamizi wa kiuchumi na kifedha walitangaza mwisho wa mamlaka makuu ya Hazina Kuu. Ushahidi na tajriba, baada ya utekelezaji wa mfumo wa urais kwa miaka 10 na ugatuzi, ni kwamba mamlaka makuu ya asasi bado yapo.

Hazina ya Kitaifa hujitengea bajeti na zile za wizara zingine, hufuatilia matumizi ya fedha kwa misingi ya bajeti iliyoweka, huendesha ukaguzi wa ndani wa matumizi ya fedha ilizotengewa na zile zilizotengewa wizara zingine na ndiyo "mzazi" wa mkaguzi wa nje - Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa hivyo, hakuna uhuru kati ya wanaopeana rasilimali, wanaotekeleza miradi, na wanaosimamia utekelezaji wazo.

**Wiki jana, kundi hilo liliagiza wakuu wa shirika hilo wafike mbele yake kuhusu tishio la marubani kugoma. Kundi la Ndii pia lilitaka kujua matokeo ya hatua ambayo sharti itekelezwe chini ya mpango uliopendekezwa na Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF) ikiwemo kupunguza gharama ya kukodisha ndege, kupunguza wafanyakazi na gharama ya mafuta.**

Kuundwa kwa asasi hizi katika Ikulu ni mwanzo tu wa mabadiliko katika mpango wa usimamizi wa masuala ya kifedha yanayotarajiwa kushuhudiwa nchini.

Serikali bado inaendesha mfumo wa kale wa uhasibu ambao hauambatani na mfumo wa kisasa.

Serikali haijahifadhi sajili ya mali, hata inapoendelea kununua mali nyingine.


Na huku ripoti za kifedha zikijumuisha mapato, matumizi ya fedha na ufadhili, zinaandaliwa kwa kuzingatia misingi ya pesa tasilimu.

Hakuna mfumo wa kuripoti masalio ya matumizi ya fedha na malimbikizo ya madeni ni suala la kudumu.

Na ingawa serikali inaendesha mfumo wa usimamizi wa fedha kieletroniki (IFMIS), mfumo huo haujashirikishwa vizuri kwa misingi ya data kwenye rekodi za kifedha.

Hii ndiyo maana ripoti za kila mara za kifedha, na ufichuzi, zimesalia changamoto kubwa. Usimamizi wa usambazaji wa pesa pia umekuwa tatizo kubwa.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*



Dkt Kamau Thugge, ambaye alihudumu katika Wizara ya Fedha kama Katibu wa Kiuchumi na Katibu Mkuu, sasa anashikilia wadhifa wa mshauri mkuu na Mkuu wa Afisi ya Masuala ya Fedha na Bajeti.

Nation Media Group "ePaper Copy"

MAGEUZI YA KIUCHUMI

# SHIDA YA IMF YAENDELEA

*Serikali mpya ya Rais William Ruto imejipata katika hali isiyoweza kuepuka inayotokana na mpango wa miezi 38 wa IMF uliokitwa katika masharti magumu yanayohitaji mageuzi yasiyo maarufu kisiasa katika sekta kadhaa*

## DAWA CHUNGU YA IMF

### Kurejesha Kenya Power katika hali ya kupata faida

Mazungumzo na IMF yanahusu kurudisha uwezo wa kifedha wa Kenya Power. Ni maoni ya shirika hilo kuwa, ingawa utathmini wa kampuni katika mwaka wa 2022 ulionyesha hatua zimepigwa katika kupunguza gharama, njia endelevu ya kupata faida bado haijapatikana.



### Kupanua ukusanyaji ushuru

IMF imeunga mkono hatua ya Kenya ya kutoza ushuru bidhaa muhimu na huduma kama gesi ya kupikia na ada za mikopo ya benki, ikisema pesa zaidi zinazokusanywa zimesaidia kukinga Wakenya na gharama ya juu ya mafuta na mbolea kufuatia vita nchini Ukraine. Inasema hatua muhimu za sera "zimeimarisha" ukusanyaji wa ushuru.




### Kuondoa ruzuku za mafuta

Mwaka huu IMF iliweka masharti mapya ya mikopo kwa kuitaka Kenya kuondoa ruzuku ya mafuta kufikia Oktoba. Hatua hiyo iliwekwa chini ya mpango wa miezi 38 wa kusaidia bajeti, katika mageuzi yaliyoambatishwa na mkopo wa Sh270.2 bilioni (dola za Amerika 2.34 bilioni).



### Mageuzi katika Kenya Airways

Kenya Airways ilikopa jumla ya dola za Amerika 841.6 milioni kutoka Exim Bank ya Amerika kununua ndege saba na injini moja. Kati ya pesa hizo, serikali ya kitaifa ilidhamini dola za Amerika 525 milioni. Kenya Airways ilishindwa kulipa sehemu ya mkopo iliyodhaminiwa na pia isiyokuwa imedhaminiwa.



### Kuchapisha ripoti ya uchunguzi wa matumizi ya pesa za Covid-19

Tangu kuzuka kwa janga hilo, IMF imeendelea kutatua shida za utawala na ufisadi katika nchi wanachama. Mnamo Mei 2020, shirika hilo lilitoa dola za Amerika 739 milioni kama mkopo usiotozwa riba kusaidia Kenya kukabiliana na athari za janga la Covid-19. Hii ilisaidia kukidhi gharama ya matumizi zaidi katika afya, kinga ya jamii, na kuharakisha malipo ili kupiga jeki uchumi.



### Kuchapisha majina ya wamiliki wa kampuni zilizopewa kandarasi

Mnamo 2018, IMF iliidhinisha Mfumokazi wa Kuimarisha Ushirikiano kuhusu Utawala. Utathmini wa muda kuhusu utekelezaji wake unaonyesha kuwa IMF ilikuwa na mazungumzo ya kina na wazi zaidi na nchi wanachama kuhusu mageuzi na masuala yanayohusu utawala na kupigana na ufisadi.



### Kubadilisha mfumokazi wa kisheria wa kukabiliana na ulanguzi wa pesa

Kenya imeharamisha ulanguzi wa pesa chini ya Sheria ya Dawa za Kulevya ya 1994.





Mkurugenzi Mtendaji wa IMF Kristalina Georgieva.

NA JAINDI KISERO

Shirika la Fedha Duniani (IMF) linataka Kenya ilipatie pendekezo kuhusu jinsi inapanga kulipa mkopo mkubwa wa dola za Amerika 2 bilioni wa Eurobond ambao unafaa kumalizwa kulipwa katika miezi 18 ijayo.

Watu walio karibu na mazungumzo na ujumbe wa IMF unaozuru Nairobi, waliambia Darubini ya Wiki IMF inapinga wazo la serikali la kuunda hazina ya kulipa mkopo wa Eurobond ambao unafaa kumalizwa kulipwa 2024.

Imeibuka kuwa msimamo wa IMF ni kuwa hazina ya kulipa mikopo ya Eurobond ambayo wakati wake kulipwa unamalizika 2024 itamaanisha inaongeza riba katika kundi moja la wakopeshaji juu ya wengine na kuwa hii itakuwa sawa na ukiukaji wa kimsingi wa kulinganisha wakopeshaji. Muda wa kulipa Eurobond wa 2024 ni hatari inayonukia na kwa sasa ni changamoto kubwa kwa Kenya katika mpango wake wa kulipa madeni ya nje.

Kulingana na takwimu za hivi punde za deni, makadirio ni kuwa, kutokana na kumalizika kwa muda wa kulipa mikopo ya Eurobond 2024, deni la nje ya litaongezeka karibu mara mbili ya kiwango cha kila mwaka - na kuwa Sh475.5 bilioni ndani ya miezi 18.

Hali hii inaweza kulazimisha serikali kurudi kutafuta mbinu mpya za kulipa deni kubwa ambazo zitakubaliwa na taasisi za kimataifa za kukopesha pesa.

Mwaka jana, Wizara ya Fedha il-

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

# Sh305 bilioni

Kulingana na ripoti ya kila mwaka kuhusu deni la nchi iliyochapishwa wiki mbili zilizopita na Wizara ya Fedha, jumla ya ulipaji wa deni la kigeni - ulipaji wa pesa zilizokopwa na ulipaji wa riba - kwa deni la serikali kufikia mwisho wa Juni 2022 lilikuwa Sh305.6 bilioni, ikilinganishwa na Sh234.5 bilioni mnamo Juni 2021. Ulipaji wa deni la nje kwa mashirika makubwa ya kimataifa ulikuwa Sh51 bilioni, ukopaji kati ya nchi mbili ulilipiwa Sh101.9 bilioni na mikopo ya kibiashara ikalipwa Sh151.8 bilioni.

ianzisha mazungumzo na wadau wa madeni ya kibiashara ikitaka kuyajadili upya na kufanyia mabadiliko mikataba ya mikopo hiyo.

Lakini mipango hiyo haikufaulu kufuatia mabadiliko katika masoko ya kimataifa yaliyosababisha viwango vya riba kwa madeni makubwa kuongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na kuzuka kwa vita nchini Ukraine.

Wizara ya Fedha ililazimika kuahirisha utekelezaji wa mpango huo. Kulingana na ripoti ya kila mwaka kuhusu madeni ya nchi iliyochapishwa wiki mbili zilizopita na Wizara ya Fedha, jumla ya ulipaji wa deni la kigeni - ulipaji wa pesa zilizokopwa na ulipaji wa riba - kwa deni la serikali kufikia mwisho wa Juni 2022 lilikuwa Sh305.6 bilioni, ikilinganishwa na Sh234.5 bilioni mnamo Juni 2021.

Ulipaji wa deni la nje kwa mashirika makubwa ya kimataifa ulikuwa Sh51 bilioni, mikopo kati ya nchi mbili ukalipiwa Sh101.9 bilioni na mikopo ya kibiashara ikalipiwa Sh151.8 bilioni. Kuongezeka kwa pesa zinazolipiwa deni la nchi za nje kunahusishwa na kuisha kwa muda wa kulipa deni (DSSI) ambao Kenya ilipewa wakati wa kilele cha janga la Covid-19.

Mnamo Aprili 2021, IMF ilikubali kukopesha Kenya wa dola za Amerika 2.3 bilioni ambao ulijiri na masharti makali, ikiwemo hatua mahsusi za kuimarisha na kuboresha usimamizi wa deni la umma.

Masharti ya kulipa deni chini ya mpango huo yanajumuisha kupunguzwa kwa kiwango cha juu cha deni la umma, viwango vya juu vya dhamana mpya kwa serikali za kaunti na mashirika ya serikali na viwango vya juu vya kuchukua mikopo mipya kutoka nje.

Kuhusu mikopo iliyodhaminiwa na serikali kwa mashirika yake, pengine mambo yanayotatiza zaidi ni masharti ya wakopeshaji kuhusu ulipaji wa deni la kigeni wa kampuni ya kitaifa Kenya Airways na Kenya Power.

Mwaka jana, Baraza la Mawaziri liliamua kujadiliana na wakopeshaji kuhusu mpangilio ambao malimbikizi ya deni la Kenya Airways yangeondolewa kupitia hatua mpya wa kuhamisha deni.

Kenya Airways ilikopa jumla ya dola za Amerika 841.6 milioni kutoka kwa Exim Bank ya Amerika kununua ndege saba na injini moja. Kati ya pesa hizi, serikali ya kitaifa ilidhamini dola za Amerika 525 milioni. Kenya Airways ilishindwa kulipa sehemu iliyodhaminiwa ya mkopo na pia ambayo haikudhaminiwa. Serikali ya kitaifa iko katika harakati za kuhamisha deni.

Kuhusu Kenya Power, mazungumzo na IMF yanahusu kuimarisha hali ya kifedha ya kampuni hiyo. Ni maoni ya shirika hilo kuwa, ingawa utathmini wa 2022 ulionyesha hatua zimepigwa katika kupunguza gharama, njia endelevu ya kupata faida bado haijapatikana kutokana na masuala kadhaa, ikiwemo kiwango kikubwa cha pesa inazolipa na inazopokea, zikiwemo zinazotoka kwa serikali kwa mpango wa kuweka stima maeneo ya mashambani.

Kuhusu kupunguzwa kwa ada mwezi Januari kulikoathiri Kenya Power, maafikiano katika mazungumzo na IMF ni kwamba kuongezwa kwa ushuru kunafungua mianya mipya ya kufilisika kwa kima cha Sh26.3 bilioni kwa mwaka.

Duru ziliambia Darubini ya Wiki kuna dalili za IMF kusukuma serikali kuchukua hatua ambazo si maarufu kisiasa za kuongeza ushuru Januari kuzuia kampuni hiyo kufilisika.

Serikali mpya ya Rais William Ruto imejipata katika hali isiyoweza kuepuka kutokana na mpango wa miezi 38 wa IMF ambao umekitwa katika masharti magumu yanayohitaji mageuzi yasiyo maarufu kisiasa katika sekta kadhaa.

Masharti hayo yanajumuisha kuongezwa kwa sehemu za kukusanya ushuru, viwango vya juu vya akiba ya nchi, kuondoa ruzuku za mafuta, kufanyia mageuzi Kenya Airways, kurejesha uwezo wa muda mrefu wa kifedha wa Kenya Power, kuchapisha ripoti ya uchunguzi wa matumizi ya pesa za Covid-19, kuchapisha majina ya wamiliki wa kampuni zilizopewa kandarasi za umma na kubadilisha kabisa mfumokazi wa kisheria wa kukabiliana na ulanguzi wa pesa.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*


**Mwaka jana, Wizara ya Fedha ilianzisha mazungumzo na wadau wa madeni ya kibiashara ikitaka kujadili upya na kufanyia mabadiliko mikataba kuhusu mikopo hiyo. Lakini mipango hiyo haikufaulu kufuatia mabadiliko kaika masoko ya kimataifa ambayo yalisababisha viwango vya riba kwa madeni makubwa kuongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na kuzuka kwa vita nchini Ukraine. Wizara ya Fedha ililazimika kuahirisha utekelezaji wa mpango huo.**



Waziri wa Fedha Njuguna Ndung'u.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# habari kwa picha



Aliyekuwa Rais wa Amerika Barack Obama amkumbatia Seneta Catherine Cortez Masto wakati wa kampeni jijini Las Vegas kabla ya uchaguzi wa kati ya muhula. PICHA | AFP



Rais William Ruto, naibu wake Rigathi Gachagua (wa pili kushoto) na Waziri wa Ulinzi Aden Dualle wazungumza na askari wa Jeshi la Ulinzi Kenya wanaojiandaa kwenda katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kama sehemu ya Kikosi cha Jumuia ya Ukanda wa Afrika Mashariki katika Kambi ya Kijeshi ya Embakasi mnamo Novemba 2. PICHA | AFP




Tingatinga lililorembeshwa kwa malenge likiwa nje ya 'Ernas Haus', makao ya wanafunzi yaliyotengenezwa upya kutokana na jengo la zamani jijini Dornbirn, jimbo la Vorarlberg, magharibi mwa Austria. PICHA | AFP



Polisi wa kupambana na ghasia wajiandaa kuondoa kizuizi kilichowekwa na wafuasi wa Rais Jair Bolsonaro katika barabara kuu ya Castelo Branco, nje ya jiji la Sao Paulo, Brazil, mnamo Novemba 2. PICHA | AFP



Mgeni akijaribu usanikishaji wa kisanii wa kuzama, wasilianifu na wa kufikiria jijini Toulouse, Ufaransa, Novemba 1.



Jowali Kitagenda arusha wavu wake kuvua samaki katika Mto Nile, mjini Jinja, Uganda, mnamo Oktoba 7. Ripoti iliyochapishwa na Taasisi ya Nile Basin mwaka uliopita ilifichua kuongezeka kwa uchafuzi wa mto huo kutokana na uchafu wa viwandani huku kanuni zikiruhusu viwanda kujengwa mita 100 kutoka kwa ukingo wa mto huo. PICHA | AFP




Mlinzi wa timu ya Paris Saint-Germain (PSG), Sergio Ramos (kulia) apigania mpira na Arkadiusz Milik wa Juventus wakati wa mechi ya Ligi ya Mabingwa jijini Turin, Italia, mnamo Novemba 2. PSG ilishinda 2-1. PICHA | AFP

Nation Media Group "ePaper Copy"

Jukwaa La

# Vijana











# KILIMO TEKNOLOJIA

*Synnefa, kampuni ya teknolojia ya kilimo, imejenga nyumba za vioo zinazotoa data za unyunyuzaji na ukulima kwa benki na vyama vya akiba na mikopo ili wakulima waweze kupata mtaji*

NAFASI YA VIJANA

# BORESHA KILIMO

**Uwekezaji:** Watu wengi wanaoshiriki kilimo ni wakulima wadogo wanaotumia vifaa duni, hali inayowachosha sana

• NA SAMMY OJWANG'

Kikitajwa kuwa nguzo kuu ya ukuaji wa uchumi nchini, kilimo kimeleta matokeo mseto miongo kadhaa iliyopita. Kabla ya uchaguzi mkuu wa Agosti, kiliibukia kuwa ajenda kuu ya kampeni ya mrengo mmoja wa kisiasa, kikiutaja kuwa suluhisho linalohitajika ili kufufua uchumi wa nchi.

Tuliambiwa kinachohitajika ni kulainishwa kwa uzalishaji katika sekta ya kilimo, kinyume na msimamo wa mrengo pinzani, ulioshikilia kuwa kinachohitajika kufufua uchumi ni kuanzishwa kwa viwanda vya kutengeneza bidhaa.

Idadi kubwa ya wakulima ni wanaokuza mazao ya matumizi ya nyumbani katika mashamba yao madogo. Wanazalisha mazao sawa mwaka mzima, kama walivyofanya mababu zao. Huwa hakuna upanzi wa mazao katika maeneo tofauti, utathmini kuhusu ubora wa mchanga, ubora wa mbegu na matumizi madogo sana ya mbolea.



Kundi la pili ni la wakulima wanaomiliki mashamba makubwa, wakitumia mitambo na mbinu za kisasa kuongeza uzalishaji. Baadhi huuza mazao yao moja kwa moja kwenye masoko na maeneo yanakoboreshwa, huku wengine wakiwafaidi mawakala wenye tamaa.

Mkulima dijitali ni suala jipya ambalo limeibuka katika kilimo. Si lazima aguse mchanga anapolima au hata kufika shambani. Wakati mwingine, huwa anajua tu mahali shamba lake lipo kupitia ramani za mtandao wa Google.

Tumeona wakulima dijitali wakipata faida kubwa kutokana na kilimo cha ngano na shayiri katika Kaunti ya Narok, wakiwa bado katika afisi zao jijini Nairobi. Utata hutokea katika furaha anayopata mkulima wa kawaida anapoanza kilimo biashara bila kupanua ardhi yake au matumizi ya mitambo.

Mkazi wa kijijini anakutana na mhudumu wa uuzaji kutoka kwa shirika la kilimo, anayemshawishi kuanza kilimo cha biashara ili kumletea pesa nyingi.

Anaanza kilimo kinachohitaji kazi nyingi ya mikono. Inalazimu familia nzima kushiriki. Katika msimu wa kwanza, kuna fedha za kutosha kugharamia karo. Pia, wanafanikiwa kujenga nyumba nzuri. Hilo ni hadi pale mkulima anapobaini kuwa hana chakula; shamba lake lote limo chini ya zao analouza, ambapo wakati wake wa kukomaa huwa mrefu.

Ikizingatiwa kampuni huwa tayari imesajili wakulima wengi kuwa wanachama wake katika eneo husika, huwa inaendelea kufurahia mapato mazuri kupitia gharama inazowekea wakulima, kama mbolea na mbegu za bei ya juu.

Malipo hulingana na ubora wa mavuno. Malipo hayo huamuliwa na kampuni baada ya kutoa mikopo inayowadai wakulima. Hofu ya wakulima wengi huwa hasara zinazoibuka wakati wa kusafirisha mazao yao.

Hadithi ya kusikitisha kuhusu kilimo cha tumbaku katika Kaunti ya Migori wakati mwingine inachekesha. Wakulima walianza kuathiriwa na makali ya kilimo cha zao hilo bila kujua. Wengi walianza kuugua kutokana na kazi walizofanya kutunza mmea huo.

Kazi hizo zinahusisha kutayarisha ardhi, nasari, kupanda mbegu, kukata miti mingi ili kutumika kama kuni, kujenga vyumba maalumu cha kuhifadhia zao hilo na kulainisha kwa moto. Moshi wa tumbaku uliwaathiri wakulima wengi.

Mkulima huyo alijipata katikati ya vita baina ya kampuni mbili za tumbaku. Kampuni iliyoanza kilimo hicho ilibaini mshindani wake alikuwa amekita kambi katika eneo hilo, akivuna mahali ambako hakuwa amepanda.

Kampuni hiyo mpya ilikuwa ikiwalipa wakulima vizuri kuliko mtangulizi wake, huku ikiahidi kuwasaidia kulipa mikopo waliyodaiwa. Hilo ni kulingana na iwapo mkulima alitaka kusaidiwa kulipa mkopo wake.

Baada ya kugundua njama hizo, kampuni hiyo ilivamia makao ya wakulima walioshirikiana na kampuni mpya kwa kutumia vijana. Ililwalazimu wengi kutoroka makwao, kwani walikuwa wametumia fedha walizopata kupitia mavuno. Hivyo ndivyo kilimo cha tumbaku kilivyosambaratika Migori.

*Bw Ojuang' ni mchanganuzi wa masuala ya kijamii.*

*Je, wewe ni kijana na mwenye maono? Tungependa kusikia sauti yako. Tuma maoni na mitazamo yako kuhusu masuala ibuka kwa:* ***weeklyreview@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

## WANAVYOSEMA



**Margaret Wangui**

Kazi Mtaani ni mpango uliowafaidi wengi. Upanzi wa miti hauwezi kuendeshwa kutokana na hali ya kiangazi inayoendelea nchini. Kwa mpango wa ujenzi, unawafaa tu watu wenye nguvu, hivyo huenda ikawa vigumu kwa wanawake wengi kujiunga nao. Hayo yatakuwa maonevu. Namuomba Rais William Ruto adumishe Mpango wa Kazi Mtaani ili kuwafaidi vijana.

*- Mwanafunzi, Chuo cha Kiufundi cha Kabete*



**Metrine Magama**

Kuna haja ya kubuni sera endelevu zitakazobuni nafasi za kazi kwa vijana. Kama mipango ya ujenzi wa nyumba za bei rahisi na upanzi wa miti itatekelezwa kwa miaka mitano ijayo, itabuni ajira na kuboresha maslahi ya vijana. Ni wazi kuwa mipango ya Rais William Ruto itawainua mamilioni ya vijana kutokana na kiwango cha juu cha ukosefu wa kazi.

*- Mwanafunzi, Chuo Kikuu cha Moi*



**Bonventure Oduor**

Nakubaliana na Rais kuhusu hatua ya kufutilia mbali Mpango wa Kazi Mtaani, na badala yake kuwashauri vijana watafute kazi za mikono katika maeneo ya mijengo na

mpango wa upanzi wa miti utakaoendeshwa na serikali. Wafanyakazi wengi wa mikono

katika maeneo ya mijengo hukuza ujuzi wao na kuibuka kuwa wajenzi stadi. Sekta hii

itawasaidia vijana wengi wanaokabiliwa na ugumu wa maisha.

*- Wawekezaji Vijana Afrika*



**Ken Kajwang'**

Haijalishi jinsi Mpango wa Kazi Mtaani ulivyochukuliwa vibaya na watu waliofuzu kutoka vyuo vikuu. Ukweli ni kuwa uliwasaidia vijana wengi wasio na ajira. Mpango wa upanzi wa miti na ujenzi ni kazi zitakazodumu kwa muda mfupi, na hazipatikani katika sehemu zote. Kwa mfano, Nairobi kuna vijana wengi wasio na ajira na ardhi ndogo sana ya kupanda miti.

*- Chuo Kikuu cha Mt Kenya*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media


MTAZAMO WANGU

# SIRI YA KUFAULU KWA TIKTOK

**MTANDAO WA KIJAMII:** Apu hii imezipa tumbojoto kampuni za kiteknolojia za Amerika zilizodhani ufanisi wa teknolojia ni haki yao



● NA WAGA ODONGO




TikTok ndiyo apu inayoopolewa zaidi ulimwenguni na imekuwa katika nafasi hiyo kwa muda. Aidha, inatazamiwa kutwaa taji kama mtandao wa kijamii ambao watu hutumia muda mwingi kwake.

Kumekuwa na hofu kuhusu kampuni ya China iliyoanzisha TikTok, Bytedance, na teknolojia yake iliyoshinda ulimwengu na inayoonekana kuifanya apu hiyo kuwa yenye mvuto zaidi. Teknolojia hiyo yamkini inawiana vyema sana na yanayovutia watumiaji hivi kwamba huku apu nyingine zikiripoti kupungua kwa muda unaotumiwa na watu kwenye mtandao wake, watumiaji wa TikTok wanaonekana tu kutumia muda zaidi kwake.

Nikiwa nimevutiwa, niliopoa apu hiyo ili kugundua kiini. Nilishangaa jinsi ilivyoweza kuoana na uraibu wangu: bunduki kubwa kubwa na mpira wa vikapu. Nilipata video chungu nzima zilizoonyesha moja kwa moja aina zote za bunduki kwenye ulingo wa ulengaji shabaha na wachezaji wa NBA wakishereheheka magoli ya aina yake. Niliweza kufanya hivi katika muda wa chini ya dakika 20, jambo ambalo ni la kufurahisha sana.

Siri ya ufanisi wa TikTok ina uhusiano mdogo sana na mfumo wake wa kukusanya takwimu. Hakuna aliye na data nyingi zaidi kuhusu watumiaji wa mitandao kushinda Google, ambayo ni mwanzilishi wa mfumo tajika ulimwenguni wa rununu za kisasa, Android, na mwendeshaji wa mtandao mashuhuri wa kusaka maarifa duniani.

Takwimu dijitali za mapendekezo yanayotokana na usomaji wa mitambo hutegemea pakubwa data zinazoingizwa na hakuna anayekusanya habari zaidi kushinda Google.

Haiwezekani kuwa Bytedance ilifanikiwa katika nyanja ambayo imesalia kitendawili kwa Facebook na Google.

Sababu inayofanya TikTok kutamba ipo kwenye mpangilio wake. Unapoingia mtandao huo kwa mara ya kwanza, unaweza ukaepuka kueleza mambo yanayokuvutia lakini bado utaishia kuyagundua. Kuuliza mtumiaji uraibu wake ni njia mwafaka ya kufahamu anachopenda.

Unapojiunga kwa mara ya kwanza na mtandao wa kijamii wa Twitter huwa unakupatia orodha ya mambo yanayoweza kukuvutia ambayo ni sharti uchague ili kuendelea. Sasa, tuseme wewe ni mwanamme mtundu kama mimi, una haja ya video za Vera Sidika akinengua mauno, Twitter yamkini hujishughulisha kukuelekeza zaidi kwa malengo yenye uzito zaidi huku ikipendekeza siasa, utamaduni au uhandisi wa datakazi.

Baada ya kuteua mada hizi, ambazo hakuna hata moja inayomuonyesha Vera, namaanisha Vera yule wa zamani si huyu mpya, mwenye makalio ya kutamanisha yaliyopunguzwa, unazabwa na misururu ya jumbe ambazo huna haja nazo.

Ni sharti ujitafutie namna ya kujinasua kutokana na mtanziko huo kwa kumfuata Vera, kubonyeza picha zake zinazokuvutia na kuchangia kila ujumbe anaochapisha ili mfumo ufahamu kukuonyesha picha zake zaidi.

Kufuata watumiaji kwenye Twitter pia hakusaidii. Hakuna mtu anayechapisha yale unayopendelea tu, bali mkusanyiko wa maoni mbalimbali. Unaweza ukamfuata Rais kwa sababu ya "mfumo wa maendeleo yanayoanzia mashinani" lakini uishie kupata misururu ya mikutano ya maombi ya ufufuo katika Ikulu.

Kwenye TikTok, hiari ya mtumiaji inajikita kwenye video moja. Inacheza na una hiari: kama huipendi unaweza ukaipuuza. Kama hautafanya chochote itacheza kwa kujirudia. Video nyingine kuhusu mada zinazohusiana pia zinaopolewa unapoendelea kutazama ili kukuepushia madhila ya msongamano wa data. Kutegemea na kasi yako ya kuamua kupuuza video husika, mfumo wake unaweza kung'amua unavutiwa na mada fulani kwa kiasi kipi.

Fikiria Facebook, Twitter na Instagram. Matini yake huwasilishwa kwenye tasnia inayojumuisha jumbe kadhaa. Pengine ujumbe wa kwanza ni kitu kinachonivutia na nyingine mbili ni jumbe zisizomuonyesha Vera, ambazo hazinivutii. Matokeo ni kudurusu na kupuuza orodha yote ya jumbe zinazoonekana ili kupata ninachopenda.

Mfumo wake haujui ni nini kati ya jumbe tatu nilizoona nilipoingia kwenye mtandao huo nilipenda au kutopenda ila tu kama nilitangamana moja kwa moja na ujumbe. Kuna ishara ndogo kuhusu ni jumbe zipi ninazofaa kuonyeshwa siku za usoni.

Kwenye TikTok, kila video ni kura kuhusu uraibu wangu ambayo ni sharti nipige au iendelee kucheza kwa mviringo usiokoma. Badiliko hili dogo limesababisha mfumo wake wa teknolojia kupata ishara bora zaidi kuhusu yanayovutia watumiaji wake.

Baada ya kuacha video icheze mara kadhaa, mfumo wake unafahamu kuwa ninapenda Vera, na utanionyesha video nyingine zaidi kumhusu katika siku za usoni.

Uvumbuzi huu ndiyo sababu kuu ya Instagram kubadilisha tasnia yake ili ifanane zaidi na TikTok.

Muundo wa matini pia ni muhimu. Kiini cha Twitter kung'ang'ana kufikia TikTok ni kuwa sehemu kubwa ya matini hapo ni maandishi. Maandishi ni ya wasomi; yanakuhitaji ufahamu kusoma, na binadamu anaweza kutafsiri picha kwa haraka zaidi. Video, kwa upande mwingine, zipo kwenye kilele cha mpangilio wa matini.

Tatizo lingine ambalo yamkini TikTok inasuluhisha ni kuzingira watu na mambo yanayowavutia. Mara tu inapofahamu unachopenda, utakuwa unaona tu Vera akinengua mauno.

*Bw Odongo ni Mhandisi wa Kompyuta*
***wagaodongo@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

KILIMO KISASA

# KUPALILIA TEKNOLOJIA SHAMBANI

**KAPU LA CHAKULA:** Synnefa, kampuni ya teknolojia ya kilimo, imejenga nyumba za vioo zinazotoa data za unyunyuzaji na ukulima kwa benki na vyama vya akiba na mikopo ili wakulima waweze kupata mtaji

• NA EDDY ASHIOYA

Kuna vitu vitatu vinavyofanya Wakenya kuwa Wakenya. Kwanza, tunateremka Mombasa mwezi Desemba, iwe tulikuwa tumepanga au la, kwa sababu Mombasa ni raha. Pili, tunapuuza ufanisi wetu, hata wakati mifuko yetu inajaa manoti ya pesa.

Lakini hatari zaidi, tumejenga mazoea ya kuiga ufanisi (au kufeli), kwa kufuata mbinu za wengine, iwe ni kuhusu mtindo wa kisasa wa mavazi, kudanganya katika mitihani (mwakenya) au biashara. Mmoja akifaulu kufungua kioski, sote tunafungua vioski.

Huo ndio msingi wa mazungumzo ambayo ninafanya na Taita Ng'etich mwenye umri wa miaka 29, mwanzilishi wa Synnefa. "Kuiga kunaonyesha tunataka kutumia njia za mkato kutufanya tufaulu. Tatizo ni, hatuweki tofauti." Aha.

Kwa hivyo, ni suala la uigaji kuwa aina ya kutaka kupata sifa? Lakini hii haiwezi kukufikisha mbali, ninalalamika. "Kwetu sisi, jinsi tunavyofanya kujitofautisha ni kwa kuweka mkulima katikati. Kilimo ni kazi ngumu, kwa hivyo tunakifanya kuwa rahisi. Huo ndio mwongozo wetu."

Synnefa ni kampuni ya teknolojia ya kilimo inayotoa suluhu za programu za kompyuta na zisizokuwa za kompyuta kuwezesha wakulima kuwa wastahimilivu.

"Nilichoshwa na kupiga simu nyumbani kutumiwa pesa za matumizi na nikaanza kutafuta shida za kusuluhisha na kupata pesa," Taita anakumbuka siku za awali. Inaibuka kuwa shida ilikuwa inamkodolea macho. Aliyekuwa akiishi naye chumba kimoja chuoni alikuwa akipanda nyanya Oloitokitok. Naye, ilivyo kawaida ya Wakenya alimuiga.

Walivuna mara moja na wakahisi walikuwa na kitu kizuri cha kufanya. Hata hivyo, mavuno ya pili yaliharibiwa na wadudu. Ya tatu, mafuriko. Mambo yalikuwa yameharibika.

Basi waliacha? Sio hasa. Aliwazia mambo ya nyumba ya kioo," anavyopenda kuyaita. Alirudi Kericho, akatafuta ploti kuanzisha moja na akafaulu katika mavuno ya kwanza. Kitu kimoja kizuri huwa kinazaa kingine na hivyo ndivyo majirani wake, pia walianza nyumba za vioo.

Nyumba hiyo ya kioo ilikuwa imetatua mambo kadhaa: hali ya hewa isiyotabirika, wadudu na vitendo vingine vya Mungu.

Lakini kilichomshangaza Taita ni shida ya wakulima kupata pembejeo bora za shambani. Kwa sasa, Synnefa ina nyumba za vioo zinazotoa data za unyunyuzaji na ukulima kwa benki na vyama vya akiba na mikopo ili wakulima waweze kupata mtaji.


"Tulijenga, kutoka chini kwenda juu, mfumo wa sola ulio na setilaiti ya intaneti ili tuweze kukusanya data kutoka shambani na kuzitumia kukopesha wakulima."

"Vijana wanataka kulima na kuwa sawa bado. Basi ni lazima kilimo kiwe cha kisasa, na hii ndiyo sababu tunabadilisha nadharia.

Siku hizi, hata kuna droni za kukagua mashamba na kufuatilia mimea. Teknolojia inafanya kilimo kuwa biashara. Ina hatari zake lakini ni lazima ujifunze jinsi ya kukabili hatari hizo."

Akionyesha data hizo, anasema wateja wa Synnefa ni watu walio na umri wa kati ya miaka 30 na 40.

Ni kweli kabisa. Taita Ng'etich ni kiumbe wa kisasa. Siku zake zilizopita zinaweza kuelezewa kwa ufupi sana. Alikulia Kericho, alikojifunza subira katika kilimo.



Taita Ngetich, mwanzilishi wa Synnefa, kampuni ya kilimo cha kutumia teknolojia inayosaidia wakulima kusuluhisha shida zao pamoja na kuwa wavumilivu. PICHA | EDDY ASHIOYA

Subira katika kilimo. Kisha akajiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi kusomea taaluma ya uhandisi ambayo ilifuatiwa haraka na kozi ya uongozi na ubunifu katika Taasisi ya Teknolojia ya Massachusetts (MIT). Katikati ya hapo alikuwa Mandela Washington Fellowship mwaka wa 2016.

Kwa sasa anasomea digrii yake ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Warwick. Mwanamume aliye mahiri wa kufanya mambo tofauti kwa wakati mmoja. Lakini ni wakati akiwa Chuo Kikuu cha Nairobi ambapo kwa mara ya kwanza alikwaruzwa na makucha ya kufeli.

Ili kuongeza pesa zake za matumizi, alianza kulima nyanya akiwa chuoni na akapata, kisha akapoteza Sh45,000. Kwa mwanafunzi, hizo ni pesa nyingi sana. Lakini ingawa kwa baadhi ya watu kufeli kunaweza kuwa ugumu kwao, kwa Taita ni sababu ya kusonga mbele.

Kilimo, anasema, nusura aachane nacho. Marafiki wake wanne kati ya sita walikiacha. "Tuna desturi ya kukumbatia kufeli; kunafaa kuwa msingi wa kujifanya bora." Hicho ndicho alichukua na kupanda katika Synnefa. Kama serikali ingemsaidia, anasema, basi sekta ya kilimo ingekuwa kapu la zawadi linaloendelea kutoa. Taita, unahisi kwamba, sio mtu wa kuvunjika moyo na anaweza kuzungumza sana ukimpa nafasi.


"Idadi ya watu inaongezeka, na tunahitaji kula lakini mabadiliko ya tabia nchi yanatuambia hatuwezi." Tunachokosa, anasema, ni usaidizi wa serikali kusukuma utengenezaji wa sera katika kiwango cha soko. Kizingiti kikubwa zaidi ni serikali.

Serikali ni mafuta yanayolainisha injini ya Kilimo. Basi, anaweza kufikiria kuwa mwanasiasa? Ninamaanisha tayari anajiamini kama mtu tajiri sana katika biashara. "Hapana," anacheka, akikumbuka wakati wa mwisho wazee wa kijiji walimuomba agombee uongozi wa kisiasa. "Siasa na ujasiriamali ni njia za kupata riziki; wajasiriamali hubadilisha dunia na kuifaidi lakini tumechagua kusifu Baranabas badala ya Yesu."

Mengi ya majibu ya Taita sio kujipiga kifua kama mjasiriamali lakini yanavuta hisia. Ukulima sio ushamba. Mimi sifichi kitu. Kutounga mkono upande mmoja wa kisiasa bado ni kushiriki siasa. Huu ndio msimamo wake: ambao ni kukwepa kitu sahihi na ajabu.

Synnefa, ananieleza, kwa wakati huu inaajiri watu 27, walio Kenya na India (am-

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media




**Maelezo kwa mchoro kuhusu jinsi Synnefa inapima mchanga kusaidia wakulima kuzalisha chakula.**



**Wafanyakazi wakipanda miche katika shamba linalosaidiwa na Synnefa.** PICHA | EDDY ASHIOYA



**Fundi wa Synnefa akiweka paneli ya kawi ya jua kutoa stima shambani.** PICHA | EDDY ASHIOYA



**Nyumba ya kioo ya kukuza mimea katika shamba linalosaidiwa na Synnefa eneo la la Isinya.** PICHA | EDDY ASHIOYA



**Mhandisi wa Synnefa Nessa Maina akiwa kazini.** PICHA | EDDY ASHIOYA

bako wamepata mtawishashi wa teknolojia).

Akiwa na soko la karibu wakulima 11,000 (asilimia 60 wakiwa maeneo ya mashambani), lazima anajionea fahari, sivyo?

"Ninafurahi sana kwa kuwa tumeshawishi taasisi za ukopeshaji kuwapa wakulima mtaji wa mikopo bila kuwaitisha dhamana, kwa kuangalia historia yao ya kilimo."

Hili linatuleta kwa maisha yake ya kibinafsi. Akiwa na umri wa miaka 25, Taita ameoa tayari. Naam, anacheka. Na, ananieleza, hakuna utaratibu wa kuoa. Ndoa, anasisitiza, ni mali iwapo utaichukulia kuwa hivyo, lakini inahitaji uwekezaji. Mwanasaikatrikia wa Uswizi Carl Jung alinukuliwa akisema, "Dunia itakuuliza wewe ni nani, na iwapo haujui, dunia itakwambia." Je, unajua yeye ni nani?

"Naam, kuwa mimi ni kusema jinsi hali ilivyo. Ninaamini Mungu sana na ninahakikisha ninatoa fungu la kumi na kufanya kazi nyingi ya kusaidia wasiojiweza, hata kwa njia ndogo." anasema. "Nna mtu wa kunisaidia ambaye ni mke wangu, kwa sababu, mtu asikudanganye, ujasiriamali ni kazi ngumu. Hata nimejifunza kucheza piano!"

Muuzaji Dijitali Janet Machuka pia anajua Taita ni nani. "Anaonyesha uongozi kwa kubuni mazingira ambayo wengine wanaweza kujitambua. Anatumia sanaa ya kukuacha ufanye kazi yako kama mtaalamu na kufaulu. Kufaulu kwake kama kiongozi kunaweza kupimwa na timu anayoongoza. Kufaulu kwa Synnefa ni kwa sababu ya Taita."

"Nikihisi sijafanya kazi ya Mungu, nahisi nimemkosea Mungu." Anampenda Mungu - na kwa njia hiyo kanisa - ambako anashukuru Mamlaka Hill Chapel kupitia mpango wake wa SALT Movement kwa kumlea.

"Nilipoteza baba yangu nikiwa na umri wa miaka kumi na mama yangu akaanza kutulea. Nafikiri alitumia pesa nyingi zaidi kunisaidia kutimiza ndoto zangu."

Lengo la Synnefa ni kujenga kampuni ambayo inaweza kununuliwa. "Nataka kuhalalisha wazo hili la biashara na wakati mwingine njia nzuri ya kufanya hivyo ni kupitia kununuliwa na kampuni kubwa ambayo inaweza kuipanua kote duniani."

Hii pia itampa muda wa kutekeleza mawazo mengine aliyo nayo. Majuzi, alipata ufadhili kutoka kwa mashirika kadhaa, yakiwemo Founders Factory Africa, Water na Energy for Food na Google Black Founders Fund Africa.

Tunapozungumzia mada ya pesa, kuna swali ambalo nimekuwa nikitaka kuuliza. "Ni kweli kwamba asilimia 75 ya pesa za kampuni ndogo hutumika kulipa mishahara?

"Mwanzilishi ni nani?" anauliza. "Hiyo ni dhana ya Ulaya, ambako wanajaribu na kufidia hatari ya biashara ndogo na mishahara mikubwa. Asilimia 62 ya mapato yetu yalienda kwa utafiti na maendeleo; tumejitolea kujenga mradi wa siku zijazo."

Ukulima umefunza Taita ustahimilivu. "Mimi ni kama yule mende asiyekufa hata ukimpiga mara gapi." Lakini ufanisi una gharama. "Nimepoteza uhusiano pale familia yangu (nasaba) inahisi ni kama sipatikanani. Uhusiano na watu mnaoanza nao pia huvurugika, kama nililazimika kumlipa mwanzilishi mwenza kwa sababu tulikuwa tumefikia hali ambayo hatungeendelea pamoja." Imekuwa na manufaa yoyote? "Naam, kuwa mkali kumenifanya kuwa mtu bora zaidi.

Na kuwa jasiri sana kumechangia kufaulu kwangu. Safari inahitaji watu wajasiri." Ninamsomea nukuu ya (leo) Tolstoy: 'Familia zote zenye furaha zinafanana; kila familia isiyo na furaha inakosa furaha kwa njia yake tofauti'.

"Nilipokuwa mshauri wa Synnefa," anakumbuka Machuka, "Taita aliniambia nisimuite bosi. Alisema: "Mimi ni kiongozi wa timu na sote tuko hapa kukua'."

Kwa hivyo, akiwa na miaka 29 mambo yamemwendea alivyotarajia? "Naam, ndio. Si nimeoa? Aha. Je niko mahali pazuri katika kampuni? Ndio. Mengine ni mambo mseto."

Kwake, kufaulu ni kuhesabu idadi ya watu ambao umesaidia kujitoa katika umaskini kwa njia endelevu. "Sio mimi kuwa kileleni, ni mimi kupeleka kamba chini kwa kila mtu apande juu."

Kutokufaulu, basi, ni kujaribu kadri ya uwezo wako na kufikiria hiyo haitoshi. Kujitoa katika biashara, anasema kunampa mtu mitazamo mipya. Jitenge na uende kufanya mambo mengine, kama kuchora au michezo ya kuigiza. Anapenda uigizaji. "Dunia yote ni jukwaa, na sisi sote ni waigizaji," anaonekana kuwa kama Shakespeare.

Basi kama angekuwa mmea, angekuwa nini? Dungusi Kakati, anasema, wenye miba nje ya kuufanya uishi lakini ndani ni mwororo.

Je, anakubali hapana kama jibu? "Hapana ngumu kwangu ni kupata mtaji. Lakini baadaye unafahamu kuwa hapana ni fursa. Inamaanisha rudi na ujiulize ni sehemu gani ya hapana unaweza kubadilisha kuwa ndio."

Kama mtu anayependa Mungu sana, kama kuna mstari katika Bibilia unaoeleza kwa kifupi maisha yake ni Warumi 8:32. "Kama aliweza kutupatia Mwanawe wa pekee, basi anaweza kutupatia kila kitu?"

Baadaye ninafahamu kwamba anatarajia mtoto mwezi Desemba. Mtu mwenye bahati huyu, pengine mtu mwerevu, lakini kwa kweli mtu aliyebarikiwa.

Wewe ni baba" anauliza. Hapana. Ninasema. Au, kwa sasa, bado.

***eddyashioya@g***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "ePaper Copy"

UZIMA WA KISAIKOLOJIA

# ANAHAMASISHA WATU KUHUSU AFYA YA AKILI

**TAIFA LENYE AFYA:** Dkt Dorcas Magai anashughulika kukuza afya ya kiakili na kuhakikisha Wakenya wote wanafikiwa na huduma za kisaikolojia pasipo unyanyapaa

• NA HILARY KIMUYU

Alipokuwa akilelewa karibu na Ufuo wa Dunga Kaunti ya Kisumu, Dkt Dorcas Magai alifikiri ndoto yake ya kuwa daktari ilikuwa imetokomea kabisa baada ya kulazimika kufanya kazi ya mjakazi kwa karibu mwaka mmoja na kukatiza masomo yake kutokana na ukosefu wa karo akiwa Darasa la Saba.

Lakini elimu ya msingi bila malipo ilipoanzishwa nchini mnamo 2003 na rais mstaafu Mwai Kibaki, alirudi shule, akafanya vyema na baadaye akajiunga na Shule ya Upili ya Kisumu Girls.

"Nilitembea kila siku kati ya kijiji changu na Kisumu Girls, umbali wa kilomita 7.5. Nusura niache shule tena nikiwa Kidato cha Kwanza kwa kukosa karo, lakini mhisani akaja kuniokoa na akanilipia karo yote iliyobakia.

Mama huyo wa watoto wawili anaelezea uchungu aliopitia miezi kadhaa kabla ya kujiunga na sekondari baada ya kumpoteza baba yake, tukio lililompa mshawasha wa kusomea udaktari. "Ndoto yangu ilikuwa kuwa daktari ili kumuokoa baba yangu aliyekuwa akiugua. Sikutaka kumpoteza mtu aliye karibu nami kamwe."

Kwa bahati mbaya, Dorcas hakupata alama zinazohitajika kusomea udaktari katika chuo kikuu, kwa hivyo aliamua kusomea saikolojia.

"Nilifuzu kwa Daraja la Kwanza na kujishindia uhisani wa kusomea shahada yangu ya Uzamili katika Saikolojia ya Kliniki na Uendelevu katika Chuo Kikuu cha Vrije Universiteit Amsterdam, Uholanzi."

Alisomea shahada ya Uzamifu katika chuo hicho pia. "Nilipokuwa nikiendeleza masomo yangu, niligundua haja ya kuanzisha uhamasishaji kuhusu afya ya akili."

Dkt Magai, 33, huelekeza utafiti wa afya ya akili kwa mtoto na mama, huunda vifaa vya afya ya akili, husimamia na kuwapa mafunzo watathmini wa nyanjani na huhakikisha udhibiti wa viwango vya ubora katika ukusanyaji wa jumla wa data.

Ndiye mwanzilishi wa shirika lisilo la kiserikali la Communities Mental Wellness lenye makao yake Malindi, ambapo huandika majarida na makala kuhusu afya ya akili. "Shirika langu linalenga kupigia debe uzima wa kiakili miongoni mwa watu binafsi, familia na jamii kupitia mikakati madhubuti."

Mradi wake wa Uzamifu ulihusu athari za muda mrefu za maradhi katika siku za kwanza 28 za maisha dhidi ya uwezo wa kufikiri na kusoma, na afya ya kiakili ya watoto wenye umri wa kwenda shule.

"Hasa, ninazingatia hali za watoto wachanga kama vile homa ya manjano na kiwango cha chini cha oksijeni, ambazo huenda zikaumiza ubongo wa mtoto na kuathiri ukuaji wake. Tunatumai kuchangia utambuzi wa sehemu muhimu zinazohitaji kuimarishwa ili kuboresha maisha ya watoto wanaopitia hali hizi."

Utafiti wake kuhusu athari za muda mrefu za homa ya manjano kwa watoto wachanga ilimshindia tuzo la kifahari la Mpango wa Kukuza Viongozi Waafrika katika Utafiti. Mnamo 2016, alitunukiwa Tuzo la



Dkt Dorcas Magai ndiye mwanzilishi wa shirika la Communities Mental Wellness na anaendelea na masomo ya baada ya digrii ya Uzamifu katika Chuo Kikuu cha Aga Khan.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

Royal Society Pfizer.

Dorcas aligundua kuna uwezekano mkubwa kwa kina mama walio na matatizo ya afya ya kiakili kupata watoto wenye matatizo ya afya ya kiakili, lakini pia kuwa kuwatunza watoto wanaougua maradhi ya kiakili huenda kukaathiri afya ya kiakili ya wanaowatunza. Hivyo basi pana haja ya vipimo vya mapema kuhusu afya ya kiakili na mikakati ya kisaikolojia kwa watunzaji na watoto wao ili kuboresha afya yao ya kiakili na maisha.

Dkt Magai anasema matatizo yanayojitokeza wakati wa ujana yasiposhughulikiwa vyema, kutakuwa na athari kuu baadaye maishani. "Matatizo makubwa kihisia na kitabia miongoni mwa watoto na vijana wa Kenya yana athari kubwa kwa nchi siku za usoni iwapo hayataangaziwa," anasema. "Yanachangia uwezekano mkubwa wa kuacha shule, tabia ya uhalifu, idadi kubwa ya watoto wa mitaani na ghasia shuleni."

Badala ya kujikita kwenye utafiti pekee, Dorcas aliamua kuzingatia utoaji huduma na akafungua kliniki kupitia Uzima wa Kiakili katika Jamii. "Nilipokuwa nikitangamana na wazazi, ningeweza kuona kuwa kuna tatizo kwa baadhi ya watoto wao kwa hivyo nikaamua kufungua kliniki hii," anafafanua.

"Nilipoanzisha kliniki ya kushughulikia afya ya akili, hata hivyo, niligundua kuwa watu hawakuweza kulipia huduma, na pia kulikuwa na unyanyapaa mwingi kwa waliokuja kutafuta usaidizi." Alipania kusuluhisha hali hii kwa kusambaza habari kuhusu afya ya akili kwenye tovuti yake.

Wazazi wanaweza kufanya nini ili kuhakikisha afya bora ya akili kwa watoto wao?

"Wazazi wanapaswa kujua kuwa boma lisilo na mazingira bora mwafaka litakuza mtoto mwenye matatizo. Kushuhudia vitendo vya kikatili kunaweza kuathiri ukuaji wa mtoto kihisia, kisaikolojia na hata kimwili."

> **Nilitembea kila siku kati ya kijiji changu na Kisumu Girls, umbali wa kilomita 7.5. Nusura niache shule tena nikiwa Kidato cha Kwanza kwa kukosa karo, lakini mhisani akaja na kunilipia karo iliyobakia ya elimu yangu ya sekondari.**
>
> Dr Dorgas Magai

"Dhuluma na utekelezaji wa mtoto kunaweza kukadumaza ukuaji wa akili ya mtoto na kusababisha matatizo kisaikolojia kama vile hali ya kujichukia, inayoweza kusababisha tabia za kujihatarisha kama vile matumizi ya mihadarati. Wazazi wanapaswa kujitahidi kuwa na muda wa kutosha wa kutangamana na watoto wao.

Huku wakifanya hivyo, wanapaswa kumchangamsha mtoto kwa kushirikiana naye kucheza, kusoma vitabu au kuimba."

Katika kipindi cha miaka michache ijayo, Dorcas anatumai kuwa mtafiti huru wa saikolojia. "Natumai kupenya katika nyadhifa za uongozi zitakazoniwezesha kuimarisha sera za afya ya akili katika taifa letu, kama vile kufutilia mbali sheria inayosema kujitoa uhai ni hatia. Nasubiri kwa hamu siku ambayo Wakenya wote wataweza kupata huduma za afya ya akili bila unyanyapaa."

Afisa wa Kliniki ya Afya ya Akili katika Kaunti ya Kilifi, Elias Fondo, anasema kazi ya Dkt Magai imebadilisha jamii. "Nilikuwa nikiwatuma wagonjwa kwake na baada ya miezi kadhaa ungeona mabadiliko. Tuliweza kupunguza ada ya matibabu kwa sababu wakati mwingine anachohitaji mtu si dawa bali ni kuzungumza na mtu," anasema.

Anasema kuwa, katika kipindi cha miaka michache aliyoishi Kilifi, unyanyapaa dhidi ya afya ya akili ulipungua. Badala yake, watu waliacha kuitisha dawa na walitaka kuzungumza na mtu.

Bw Peter Wanjohi, mwanzilishi wa Shirika la Brant, taasisi ya kijamii inayofanya kazi na walemavu Malindi, anasema ni vigumu kupata huduma kama vile ushauri nasaha unaohusu maradhi ya kiakili katika sehemu hiyo ya nchi lakini Dorcas amejaza pengo hilo.

"Tulikutana katika mkutano wa wanajamii ambapo tulizungumza kuhusu baadhi ya visa nilivyokuwa nikishughulikia vya watoto na vijana chipukizi walio walemavu, athari za kiakili kutokana na kutelekezwa, na mzigo kwa wazazi. Alisema atasaidia, na kila kitu kikabadilika baada ya hapo," anasema Wanjohi akiwa mwingi wa shukran.

***hkimuyu@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*




ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

taharìri




■ Kikosi cha Flying Squad kilikuwa kitengo cha wauaji maarufu. Kile cha SSU kilijipata mashakani kwa sababu hiyo hiyo

# Huduma ya silaha ni mbaya kwa sheria



KWENDO
OPANGA

Balaa iliyoje! Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP) Noordin Haji anaambia kituo cha televisheni aliwasilisha kesi dhidi ya Naibu Rais Rigathi Gachagua kwa kuzingatia ushahidi uliotungwa.

Anasema hati kiapo ambayo kesi yake ilitegemea ilikuwa bandia. Na anasema alishinikizwa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai (DCI) George Kinoti amshtaki Gachagua.

Kabla ya hili, afisa wa cheo cha juu ambaye alikuwa mdogo wa Kinoti alikuwa amedai kuwa DCI alitoa agizo kali na muda wa kukamatwa na kushtakiwa kwa Gachagua kwa kosa la uporaji wa pesa.

Matokeo ya fichuzi hizi ni kwamba wakuu wa DPP na DCI walifanikisha kukamatwa na kushtakiwa kwa mwanasiasa kutokana na sababu ambazo hazikuwa za haki.

Hapo awali, maafisa kadhaa wa polisi walikuwa wamekamatwa kuhusiana na kisa cha kiajabu na cha kushtua ambapo raia wawili Wahindi walitekwa nyara na baadaye mabaki ya miili yao yakapatikana katika Mlima Kenya.

Wawili hao walikuwa wataalamu wa teknolojia ya habari (IT) ambao inadaiwa waliletwa nchini kuhudumia Naibu Rais, sasa Rais, William Ruto, wakati wa kampeni.

Wakati huo huo kikosi hatari cha kupambana na uhalifu (SSU), ambacho polisi waliokamatwa walihudumia, kilivunjwa.

Hatua hiyo ilileta kumbukumbu ya kikosi kilichoogopwa cha Flying Squad kilichovunjwa na Kinoti 2018 na nafasi yake kuchukuliwa na SSU. Si ajabu kwamba sababu zilizochangia kuvunjwa kwa Flying Squad ni sawa na sababu ambazo zimechangia kuvunjwa kwa SSU.

Suala hili linaashiria nini kwa Idara ya Polisi nchini, tabaka la wanasiasa, usimamizi wa haki na DCI na DPP katika mashindano ya kisiasa ya kulipiziana kisasi?

Hali halisi ni kwamba polisi na utumishi wa umma hawapaswi kupendelea upande wowote katika mashindano ya kisiasa. Wajibu wao ni kuhudumia serikali kuhudumia watu.

Polisi wanapomwekelea raia kosa, wanakiuka sheria na polisi wanapokiuka sheria, basi, hakuna sheria. Polisi wakivunja sheria kwa manufaa ya wenye ushawishi wa kisiasa, basi, polisi watachukua sheria mikononi mwao na kuathiri raia kwa njia inayodunisha na kwenda kinyume na ubinadamu.

Walio mamlakani wanapotumia polisi kujifaidi, wakiondoka mamlakani, waliokuwa waathiriwa wa maovu ya polisi nyakati hizo pia watatumia polisi kutenda maovu. Haya yataishia wapi?

Shida ni wakati polisi wanapoingia katika mashindano kuunga upande wa walio mamlaka dhidi ya wanaopania kuchukua mamlaka kutoka kwao kupitia kura.

Matumizi ya Huduma ya Polisi kuendeleza maovu huendeleza dhana kwamba wajibu wa polisi ni kuhudumia mamlaka na kukandamiza umma, kwamba ni kikosi cha kudhibiti na ni huduma kwa jina tu.

Pia inaendeleza dhana kuwa kuna wakubwa na kuna raia, na polisi wapo kuweka raia mbali na wakubwa. Kikosi cha Flying Squad kilikuwa kitengo cha wauaji maarufu. Kile cha SSU kilijipata mashakani kwa sababu hiyo hiyo.

Je, kikosi kitakachofuata, bila kujali jina lake, kitakuwa tofauti? Bila shaka hakitakuwa tofauti kama wakuu wa maafisa wake na wenye mamlaka ya kisiasa wanachukulia huduma hiyo kuwa kikosi na, kibaya zaidi, chombo cha kutatua uhasama wa kisiasa.

Na kuna uhakika kwamba wananchi wataogopa maafisa wa polisi, hasa wanaovalia mavazi ya kiraia, ambao wangetaka wasaidiwe kwa habari za kuwasaidia kukamata wahalifu. Katika hali zote zilizoelezewa hapo juu, haki huumia. Kwa hivyo, huduma inayotumiwa kuendeleza maovu haiendelezi mfumo wa kupatikana kwa haki.

***kwendo58@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

Jangwa linaloenea ni uhalisia tunaoweza kuona, na tunajua maana yake kwa uzalishaji wa chakula

# Kampeni ya Ruto ya mazingira safi ni nzuri



MACHARIA
GAITHO

Tofauti na kawaida ya kiongozi wa Kenya, Rais William Ruto amefanya mabadiliko ya Tabia Nchi kuwa nguzo ya shughuli zake humu nchini na kimataifa.

Kuongeza misitu kama mkakati wa kukabiliana na ukame unaokumba eneo pana la Mashariki ya Afrika kunaonekana kupewa kipaumbele katika ajenda ya Kenya Kwanza.

Ameteua mshauri mkuu wa masuala ya mabadiliko ya tabia nchi katika afisi yake, huku suala hilo likijitokeza sana katika hotuba yake ya kwanza katika Kongamano la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mnamo Septemba, na kuvutia gazeti maarufu la New York Times.

Pembeni mwa kongamano, pia alikutana na viongozi wengine wa Afrika waliokuwa New York, ambapo alisisitiza tishio la mabadiliko ya tabia nchi kwa bara zima, hasa kwa kuharibu vyanzo vya maji, kukauka kwa mito, kupungua kwa mvua na hatimaye kuharibika kwa kilimo, bei za juu za chakula, ukame na njaa.

Hiyo ilikuwa kamati ya tatu ya Wakuu wa Nchi za Afrika Kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi (CAHOSCC), ambayo ilikuwa ikishinikiza sauti moja kabla ya Kongamano la nchi wanachama wa UN kuhusu Mfumokazi wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabia Nchi (CoP27) litakalofanywa Misri baadaye mwezi huu.

Kenya inaongoza kwa kutayarisha stakabadhi ya pamoja ya msimamo wa Afrika katika Cop27, ambayo Ruto anatarajiwa kuwasilisha, ikiwa na manufaa ya kando ambayo itaashiria kufika kwake katika jukwaa la kimataifa kama kiongozi shupavu wa Afrika na Kimataifa.

Hakuna haja ya kusisitiza kuhusu athari za ukame, inavyoshuhudiwa hapa nyumbani huku njaa ikitanda kote, mimea ikikauka mashambani, mifugo wakifa kwa kukosa maji na malisho, na raia wakiomba chakula.

Mahojiano ya Ruto na vyombo vya habari vya kimataifa katika ziara zake nje ya nchi baada ya kushika uongozi Septemba pia yalionyesha Mabadiliko ya Tabia Nchi yakijitokeza kama moja la masuala atakayopatia kipaumbele.

Serikali yake ililazimika kutenga pesa kununua na kusambaza chakula cha msaada, na kuathiri zaidi uwezo wake wa kutimiza ahadi zake za kampeni za uchaguzi.

Ruto, kwa kutambua mabadiliko ya tabia nchi ni moja ya vitisho vikubwa vinavyokabili Kenya na maeneo mengine ya Afrika, anajionyesha kuwa kiongozi anayetazama zaidi ya masuala madogo ya nyumbani, ambaye ana uwezo wa kufikiria na kuchukua hatua kimataifa, na anayetambua masuala ya humu nchini yanaunganika na matukio na shughuli nje ya mipaka yetu.

Hata hivyo, kuna wanaofikiri Ruto anahubiri maji na kunywa mvinyo. Wanataja ahadi yake ya kupanda mamilioni ya miti dhidi ya ukweli kuwa alikuwa mmoja wa viongozi wa serikali ya Muungano wa Kitaifa ya Rais Mwai Kibaki, waliopinga mpango wa aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo Raila Odinga wa kufurusha waliovamia Msitu wa Mau na kukomboa mnara muhimu wa maji Afrika Mashariki.

Uhusiano mbaya uliozuka kati ya Ruto na Raila, ambao walikuwa wameingia katika Muungano Mkuu wakiwa marafiki chini ya bendera ya chama cha ODM, unadumu hadi leo.

Ajenda ya Kenya Kwanza pia inaonyesha mtindo unaotisha. Mmoja ni tangazo la Naibu Rais Rigathi Gachagua kwamba mpango wa 'shamba system', ambao uliruhusu kilimo ndani ya misitu, utaruhusiwa tena.

Miaka mingi iliyopita mshindi wa tuzo ya Nobel mwanamazingira Wangari Maathai alifichua mpango huo kuwa uliochangia pakubwa uharibifu wa misitu.

Kuruhusu jamii maskini zilizoishi karibu na misitu kupanda chakula katika misitu na kutunza miti kuliwapa nafasi watu matajiri na wenye ushawishi kunyakua ardhi ya misitu.

Manifesto ya Kenya Kwanza, kando na kusisitiza ulinzi wa misitu, kwa kweli inahusika zaidi na matumizi ya mazao ya misituni.

Kwa mfano, hii haihusu kukata miti pekee kupata mbao kutoka misituni, lakini inafungua uchomaji wa makaa na shughuli zizodhibitiwa ambazo awali zilisababisha uharibifu mkubwa wa misitu inayopaswa kulindwa.

**Kenya inaongoza kwa kutayarisha stakabadhi ya pamoja ya msimamo wa Afrika katika Cop27, ambayo Ruto anatarajiwa kuwasilisha, ikiwa na manufaa ya kando ambayo itaashiria kufika kwake katika jukwaa la kimataifa kama kiongozi shupavu wa Afrika na Kimataifa. Hakuna haja ya kusisitiza kuhusu athari za ukame, inavyoshuhudiwa hapa nyumbani huku njaa ikitanda kote, mimea ikikauka mashambani, mifugo wakifa kwa kukosa maji na malisho, na raia wakibaki kuombaomba chakula.**

Ruto pia amelaumiwa kwa kutokuwa makini sana katika kulinda nafasi ya Kenya kama nchi ya tatu ulimwenguni inayozalisha kawi salama, hasa kawi ya mvuke, huku akielekea kuongeza uwekezaji katika makaa ya mawe, mafuta na vyanzo vingine vya nishati.

Hata kuna kinachoonekana na wengi kuwa mradi unaoshinikizwa na mitandao ya wafanyabiashara wanaolenga kujifaidi wa kujenga kiwanda cha nuklia. Bila shaka hizi sio sifa za kampeni ya mazingira ambayo Rais Ruto anavumisha katika jukwaa la kimataifa huku akifanya kinyume nyumbani.

Hapa ndipo tunafaa kumuuliza Ruto kuonyesha anachosema kwa vitendo. Kuongezeka kwa joto duniani na masuala mengine kunaweza kuonekana kuwa shida ya nchi zilizostawi kukitazamwa dhidi ya utoaji wetu wa gesi hatari angani.

Afrika haiwezi kukaribia Amerika, China, Urusi, Ujerumani, Japan, Uingereza, India na nchi zingine zilizoendelea kiviwanda kuhusiana na uharibifu wa anga na moshi kutoka kwa viwanda, magari na vituo vya kawi.

Hasa, kuna mjadala kuhusu iwapo ukame unaokumba sehemu za ardhi yetu ni matokeo ya mabadiliko ya tabia nchi, au ni mfumo wa kawaida wa mzunguko wa hali ya hewa ambao tunashuhudia ukame kila muongo au hata kila miaka 50, ukibadilishana na mafuriko ambayo yanazidi gharika ya Noah.

Vita vya kitaaluma na itikadi kando, ukweli mtupu ni kwamba tunaweza kuona athari halisi za uharibifu wa mazingira tunamoishi.

Kufungua misitu kwa kilimo kunafanya mchanga kupoteza rotuba inayosombwa mvua inaponyesha, na kuacha ardhi isiyoweza kumea au kupandwa chochote. Jangwa linalotanda ni ukweli ambao tunaona, na tunajua maana yake kwa uzalishaji wa chakula.

Kwa hivyo, sote tuunge mkono kampeni ya kimataifa ya Ruto kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi, huku nyumbani tukimfanya awajibike kwa baadhi ya mambo madogo ambayo ni muhimu. Haya yatakuwa ni kulinda na kupanua misitu, kulinda chemichemi za maji na fuo za bahari dhidi ya wanyakuzi wa ardhi, kusafisha mito iliyochafuliwa na kupunguza matumizi ya kemikali na dawa za kuua wadudu zinazofanya chakula tunachozalisha kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

*gaithomail@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

AMANI NA UTHABITI WA KISIASA KATIKA UKANDA



**Waziri Alfred Mutua anasema Wizara ya Kigeni na Masuala ya Ughaibuni itashirikiana na benki ili kuwezesha Wakenya wanaoishi ng'ambo kuweka kwa urahisi pesa katika benki nyumbani ili kuongezea kiasi cha pesa wanazotuma nyumbani kila mwaka ambacho kwa sasa ni Sh400 bilioni.** PICHA | JEFF ANGOTE

# KENYA TAYARI KWA DUNIA

*Mutua aelezea sera ya kimataifa ya utawala wa Ruto, asema Kenya inataka kutafuta masoko barani Afrika na kwingine. Kinyume na maoni ya wengi, Mutua anakana kuwa Kenya inategemea China au inaweza kuipa mali yake kwa sababu inadaiwa pesa nyingi*

• NA KWENDO OPANGA

"Mimi si mgeni hapa," anasema Dkt Alfred Mutua, Waziri mpya wa Kigeni na Masuala ya Ughaibuni. Baada ya kuhudumu kwa miaka tisa kama msemaji wa serikali ya Kibaki na mihula miwili kama Gavana wa Machakos, anaonekana kujiamini.

Ni siku yake ya kwanza afisini na wafanyakazi wanapoingia, wanashangaa wanapoambiwa kuwa Waziri aliwasili afisini mwake saa moja asubuhi.

Muda mfupi baada ya saa tatu za asubuhi, Balozi wa Saudi Arabia, Khalid bin Abdullah Al-Salman, anaelekezwa afisini mwake, hivyo kuwa balozi wa kwanza kumtembelea waziri huyo mpya. Anapojituliza kwa mahojiano haya, Mutua anafichua kuwa yatakapochapishwa atakuwa amesafiri Saudi Arabia na kurudi.

Mbona balozi wa Saudia ndiye mgeni wake wa kwanza na nchi hiyo ndiyo atazuru kwanza? Kwa sababu ya ripoti za kukera za mateso, dhuluma na hata vifo vya Wakenya wanaohudumu kama wafanyakazi wa nyumbani nchini Saudi Arabia zilizoshamiri katika vyombo vya habari na asasi za serikali.

"Ni suala la taratibu na mifumo kati ya Kenya na Saudi Arabia. Nitafanya ziara ya kufahamu ukweli," anaambia Darubini ya Wiki.

Anaeleza kwa kina. "Tumeamua na Wizara ya Leba kufanya mikutano na maajenti hapa na Saudi Arabia kisha tutachukua msimamo. Zingatia kuwa Saudi Arabia ni nchi rafiki na mshirika wetu kimaendeleo, tunahitaji kutafuta nafasi za ajira kwa wataalamu wetu huko na si wafanyakazi wa nyumbani pekee."

Hata hivyo, Mutua anataja kuwa, ingawa Kenya inahitaji Saudi Arabia kuwekeza nchini na kuajiri wataalamu wake, ni wajibu wake kuhakikisha usalama na maslahi ya Wakenya ughaibuni yanalindwa.

"Pindi unapochukua boda boda, tuk tuk, basi au ndege na kuvuka mpaka, serikali itakufuatilia na hii ndiyo sababu kuhusiana na Saudi Arabia tunahitaji kujua kinachoendelea na jinsi tunaweza kukitatua. Maslahi ya Wakenya ni muhimu zaidi."

Wema huanza nyumbani na hivyo Mutua anasema anataka maafisa wa balozi za Kenya kuwaheshimu Wakenya walio ng'ambo. "Nataka wizara hii ibadili mwelekeo wake kuhusu Wakenya wanaoishi ng'ambo. Wanafaa kushu-

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## kurunzi ya kenya



Waziri wa Kigeni na Masuala ya Ughaibuni Alfred Mutua akihojiwa na mwandishi wa *Darubini ya Wiki* Kwendo Opanga ofisini mwake jijini Nairobi mnamo Oktoba 28. PICHA | JEFF ANGOTE

ghulikiwa kwa heshima. Wakienda katika afisi za ubalozi, wanafaa kuhisi kuwa wameenda nyumbani kutokana na jinsi watashughulikiwa na matatizo yao kutatuliwa.

Moja la mabadiliko ambayo Mutua anataka kuanzisha linahusu paspoti. Kama Mkenya anataka paspoti na yuko tayari kusubiri kwa majuma mawili, Mutua anasema ni sawa. Lakini kama mwingine anataka paspoti haraka na yuko tayari kuilipia, mipango inafaa

> **Tunapeleka Kenya kwa dunia. Tunataka kutafuta masoko katika bara la Afrika na kwingine. Marafiki zetu ni marafiki zetu na maadui wako sio lazima wawe maadui wetu. Tunaweza kufanyakazi na mataifa ya Mashariki, Magharibi, Kaskazini kwa sababu kwetu suala kuu ni kwa wizara hii kuwezesha nchi kwenda mbele.**
>
> Alfred Mutua

kuwekwa kushughulikia watu kama hao "kama njia ya kutoa huduma bora na za kutegemewa kwa watu wetu."

Waziri pia anataka kuweka namna "bora kwa Wakenya wanaoishi ughaibuni kutuma pesa Kenya" na akapendekeza kuwa wizara yake itashirikiana na benki ili ziwezeshe Wakenya walio ughaibuni kutuma pesa zao nyumba kwa urahisi ili kuwezesha kuongezeka kwa kiwango cha pesa wanazotuma nyumbani "ambacho sasa ni Sh400 bilioni kila mwaka."

Anataka wizara hiyo itoe nafasi za ufadhili wa masomo kwa Wakenya wengi iwezekanavyo ili waende kusoma ng'ambo. "Nataka kuweka nguvu mpya katika mfumo huu ili watu wetu wapate ufadhili wakasome, wawezeshwe na wapate ajira kwa mpango bora wavyofanya nchini Ufilipino. Tunaweza kuwatuma maelfu ya Wakenya kufanyakazi ng'ambo."

Rais wa zamani Mwai Kibaki na mrithi wake Uhuru Kenyatta, walielekeza Kenya kwa mataifa ya Mashariki. Je, Rais Ruto na Mutua wanaelekeza Kenya kwa mataifa ya Magharibi? "Tunapeleka Kenya kwa ulimwengu. Tunataka kutafuta masoko katika bara la Afrika na nje. Marafiki zetu ni marafiki zetu na maadui wako hawafai kuwa maadui wetu. Tunaweza kushirikiana na mataifa ya Mashariki, Magharibi, Kaskazini kwa sababu kwetu suala kuu ni kuiwezesha Kenya kuendelea," Mutua anasema.

Wizara hiyo inalenga masuala mawili makuu: kuchanganya diplomasia na biashara. "Tutawapa mabalozi wetu mafunzo mapya ili wafikirie kuhusu biashara, tutawafunza wafanyakazi wetu katika balozi zetu ili wafikirie kuhusu pesa, wafikirie kuhusu masuala ya kiuchumi.

Kwa hivyo, tunapofikiria kuhusu utulivu na amani, ni sharti tusafirishe bidhaa zetu ng'ambo na bidhaa hizo sharti ziwe za ubora na viwango vinavyohitajika ili tuweze kustawisha uchumi wetu," Mutua akaambia Durubini ya Wiki.

Kwa hivyo, wizara hiyo itatekeleza wajibu mkubwa kunadi Kenya katika kitovu cha biashara na viwanda katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mpango wa serikali ni kuvutia kampuni za utengenezaji bidhaa kuja nchini ili zitumie nchini kama vituo vyake na kuifanya Kenya kuwa taifa linalouza nchini bidhaa zilizotengenezwa. "Mmoja wa wajibu wangu ni kuhakikisha nimewezesha wawekezaji kuja Kenya," Mutua anafichua.

Anasema Kenya imejitolea kuendeleza amani katika nchi za Ethiopia, Somalia, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa sababu amani na utulivu wa kisiasa katika eneo hili italeta ustawi wa kiuchumi.

Hii ndiyo sababu Kenya, anasema, inaunga mkono mazungumzo ya kisiasa kama suluhu kwa mapigano nchini Ethiopia wala sio suluhu ya kijeshi "kwa sababu hakuna washindi katika suluhu ya kijeshi."

Kulingana na waziri huyo, Kenya inaunga mkono wazo la kuunganisha ukanda huu kiuchumi kwa kusawazisha ushuru, ambapo biashara inaendeshwa kwa urahisi na hakuna tofauti kati ya anayefanya biashara mbali na nyumbani na anayefanya biashara nyumbani.

Hiyo ndiyo sababu, anasema, "ufanisi DRC, nchi iliyobarikiwa kwa miti, uwezo wa kuzalisha nguvu za umeme kutokana na maji, ardhi yenye rutuba na madini, unaweza kuwa ufanisi kwa ukanda huu.

Kinyume na ripoti za awali, Mutua aliambia Darubini ya Wiki kuwa wanajeshi wa Kenya wamepelekwa DRC kama kikosi cha kudumisha amani, wajibu ambao Kenya imejulikana na kuheshimiwa kwao tangu miaka ya 1980.

Alipoulizwa muda ambao wanajeshi wa Kenya watakaa DRC, Mutua alijibu kuwa hawa-

> **Sh400 bilioni**
>
> Pesa ambazo Wakenya wanaoishi ng'ambo hutuma nyumbani kila mwaka.

takuwa huko kwa kipindi kirefu zaidi ya inavyohitaji kwa "sababu haja yetu si kuona kuwa wanajeshi wetu wanakaa kwingine. Tunataka wafanye kazi yao kisha warudi nyumbani."

Nje ya Afrika, Waziri anasema Kenya inataka kuwa mwanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa sababu ya sifa zake kama taifa lenye amani, utulivu na lisiloegemea upande wowote.

Pia Kenya ni mwanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Afrika na imewahi kushikilia urais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, nafasi bora katika wajibu huo. Kuna uwezekano kwamba Kenya itashindania kiti hicho cha UN na mataifa kama Nigeria, Misri na Afrika Kusini.

Akirejelea dhana kwamba Kenya inategemea China au kwamba inaweza kupeana mali yake, hasa kwa sababu China inaidai pesa nyingi, Mutua anasema hivi: "Nimefanya mazungumzo na nikitazama uhusiano wetu na China, siogopi chochote. Deni letu si kubwa," anasema.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

"ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# STIMA KUTOKA ANGANI KUELEKEZWA ARDHINI



LONDON

Ni habari za kufurahisha sana ambazo huenda zikaonekana kutoaminika: mpango wa kuvuna kawi ya jua kutoka angani na kuielekeza Duniani kwa kutumia vikangazi.

Hata hivyo, ni jambo ambalo huenda likafanyika ifikiapo 2035, kulingana na Martin Soltau, mwenyekiti-mwenza wa Mpango wa Kawi ya Angani (SEI), ambao ni ushirikiano wa sekta hiyo na wasomi.

SEI inatekeleza mradi unaoitwa Cassiopeia, unaolenga kuweka msururu wa setilaiti katika moja ya njia inayofuatwa na Dunia angani. Baada ya kutumwa angani, setilaiti hizo zitakuwa zinavuna kawi ya jua na kuielekeza Duniani. Anasema setilaiti hizo zina uwezo mkubwa. "Kulingana na tafiti zetu tulizonakili, huenda ikazalisha kawi ya dunia yote kufikia 2050," akasema.

"Kuna nafasi ya kutosha kwenye vijia hivyo kwa setilaiti za kuzalisha kawi ya jua, na uwezo wa jua kuzalisha kawi ni mkubwa. Kijia maalumu ambacho dunia hupitia huwa kinapokea kawi mara 100 zaidi ya kiwango ambacho wanadamu wote wanatabiriwa kutumia ifikapo 2050," anasema Bw Soltau.

Mapema mwaka huu, serikali ya Uingereza ilitangaza ufadhili wa Sh405 milioni kwa miradi inayohusu utegaji wa kawi angani (SBSP). Hili ni kufuatia utafiti wa kihandisi uliofanywa na kampuni ya Frazer-Nash, iliyobaini kuwa teknolojia hiyo inafaa. SEI inalenga kupata mgao mkubwa wa fedha hizo.

Setilaiti zake zitatengenezwa na maelfu ya chembechembe ndogo zilizotengenezewa viwandani Duniani na kuunganishwa angani na roboti huru, ambazo zitakuwa zikidumisha hali ya setilaiti hizo. Kawi ya jua iliyokusanywa na setilaiti itageuzwa kuwa mawimbi ya redio yenye nguvu na kuelekezwa Duniani.

Mawimbi hayo baadaye yatageuzwa stima. Kila setilaiti itakuwa na uwezo wa kuzalisha karibu Gigawati mbili (2GW) za stima na kuiweka katika mfumo rasmi wa kusambaza.

Hapa duniani, miale ya jua hupunguzwa nguvu na anga, lakini angani, huwa inatoka moja kwa moja kutoka kwa juani bila mwingilio wowote.

Hivyo, kifaa cha kukusanya kawi ya jua kilicho angani kinaweza kukusanya kawi nyingi kuliko kilicho Duniani.

Miradi kama hiyo inajaribiwa kwingineko duniani. Nchini Amerika, kwa mfano, Maabara ya Utafiti ya Jeshi la Ndege (AFRL) inaendesha majaribio kwa mfumo kama huo, kwenye mradi unaoitwa Space Solar Power Incremental Demonstrations and Research (SSPIDR). Hili linajumuisha kuboresha ufaafu wa betri za kawi ya jua, kugeuzwa kwa mawimbi ya jua hadi kwa mfumo wa redio na kupunguza tofauti kubwa za joto.

Mwishoni mwa mwaka uliopita, kundi hilo lilionyesha jinsi kawi ya jua inaweza kugeuzwa mawimbi ya redio. Huenda kuwepo kwa mawimbi ya kikangazi kukazua hofu. Hata hivyo imedhihirishwa Duniani kuwa hayana madhara yoyote kwa binadamu na wanyama.

"Miale hiyo ni kama mtandao ambao huwa tunautumia kila wakati. Nguvu zake ni ndogo. Nguvu zake ni kama robo ya nguvu za miale ya kawaida kutoka kwa jua la saa sita mchana," akasema Bw Soltau. "Kama uko kwenye ikweta katika jangwa, unaweza kupata kama Wati 1,000 za umeme kwa kilomita moja mraba. Hata hivyo, hili ni robo ya kiwango hicho: karibu Wati 240 kwa kilomita moja mraba. Kwa hivyo, ni miale salama."

Ingawa vikwazo vingi tayari vimetatuliwa, bado kuna changamoto kadhaa.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# Ndoto ya China: Safari ndefu ya mwezini

China ilifaulu kuzindua muundo wa mwisho wa Kituo cha Angani cha Tiangong wiki hii, ikikaribia kumaliza ujenzi wake kufikia mwishoni mwa mwaka huu. Huo utakuwa ufanisi mkubwa katika juhudi za taifa hili kuzuru angani.

Taifa hilo limewekeza mabilioni ya pesa katika mpango huo, likitarajia hatimaye litafaulu kumtuma mwanadamu Mwezini. China imekuwa ikijaribu kufikia mataifa kama Amerika na Urusi, ambayo wanaanga wake wana tajriba ya miaka mingi katika masuala ya kutalii anga.

Huu ndio mpango wa taifa hilo wa kuruzu anga na huu ndio mwelekeo wake: Mara tu baada ya Urusi kuzindua roketi iliyoitwa Sputnik mnamo 1957, Mwenyekiti Mao Zedong alitangaza: "Sisi pia tutatengeneza setilaiti."

Ilichukua zaidi ya mwongo mmoja, ingawa mnamo 1970 China ilizindua roketi yake ya kwanza, iliyoitwa Long March. Ilichukua muda mrefu zaidi kutengeneza roketi za kusafirisha binadamu.

Mnamo 2003, Yang Liwei aliibuka kuwa mwanaanga wa kwanza kutoka China kutumwa angani. Uzinduzi wa safari hiyo ulipokaribia, hofu kuhusu usalama wa roketi hiyo zililifanya taifa hilo kusimamisha upeperushaji wa hafla hiyo moja kwa moja kupitia televisheni katika dakika ya mwisho.

Hata hivyo, safari iliendelea kama ilivyopangwa. Yang alifanikiwa kuzunguka Dunia mara 14 kupitia Roketi Shenzhou, kwenye safari iliyodumu saa 21. Tangu wakati huo, China imetuma roketi saba angani.

Kwa kufuata nyayo za Amerika na Urusi, China ilianza kupanga kujenga kituo chake cha angani kinachoizunguka dunia. Tiangong-1 lab ilizinduliwa 2011. Mnamo 2013, mwanamke wa pili kutoka China kwenda angani, Wang Yaping, alitoa mafunzo maalumu kwa watoto nchini humo kwa njia ya video kuhusu utalii angani akiwa ndani ya kituo cha anga.


*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya afrika

■ SEHEMU 10 YA SPLM INAMZUIA MAKAMU WA RAIS KUSHIRIKI SHUGHULI ZA CHAMA

# HALI SI SHWARI TENA



Rais wa Sudan Kusini Salva Kiir (kulia) na naibu wake Riek Machar wasalimiana walipoweka mkataba wa amani katika Kongamano la 33 la Mamlaka ya Serikali za Mataifa Kuhusu Maendeleo (IGAD) jijini Addis Ababa, Ethiopitia, mnamo Septemba 12, 2018.

*Taharuki ya kisiasa yaongezeka Sudan Kusini baada ya Makamu Rais Machar kutimuliwa na Rais Kiir katika chama tawala cha Sudan Peoples' Liberation Movement. Washirika wa Machar wanasema kitendo hicho kinakiuka Mkataba wa Arusha uliotiwa saini Januari 21, 2015, ambapo pande zote ziliapa kujitolea kurudisha umoja katika SPLM*

• LEVIN OPIYO

Juhudi za kupatatikana kwa amani na uthabiti Sudan Kusini zinakumbwa na changamoto nyingine, baada ya Makamu wa Rais wa taifa hilo, Riek Machar, kuondolewa kama naibu mwenyekiti wa chama tawala cha Sudan People's Liberation Movement (SPLM), kwenye mkutano ulioongozwa na Rais Salva Kiir wiki iliyopita.

Kulingana na Katibu Mkuu wa SPLM, Peter Lam Both, Machar alifukuzwa kwenye uongozi wa chama hicho kulingana na Sehemu 10 ya Katiba ya SPLM, inayosema kuwa mtu atapoteza uanachama wake mara moja anakibuni ama kujiunga na chama kingine cha kisiasa.

Kiini cha mzozo wa sasa ni chama cha Sudan People's Liberation Movement in Opposition (SPLM-IO), alichobuni Machar mnamo 2013 baada ya kuondoka katika SPLM kufuatia mvutano wa mamlaka kati yake na Rais Kiir.

Kulingana na serikali, Sehemu 10 ya SPLM inamzuia Machar kushiriki katika shughuli za chama kutokana na uhusiano wake na SPLM-IO. "Huwezi kuwa mwanachama wa SPLM na pia wewe ni mwenyekiti wa chama kingine kinachoitwa SPLM-IO; haiwezekani," akasema Katibu Mkuu wa SPLM Kuhusu Masuala ya Kisiasa, Kuol Atem. Hata hivyo, Machar na washirika wake wanasisitiza kuwa "Hakuna mrengo unaoweza kumuondoa mwanachama wa mirengo mingine kutoka SPLM," na zaidi, SPLM-IO si chama cha kisiasa kilichosajiliwa.

Wanashikilia kuwa kufurushwa kwao kutoka chama hicho kunakiuka Mkataba wa Arusha uliotiwa saini Januari 21, 2015, ambapo pande hizo mbili zilikubali kujitolea kuunganisha SPLM na makundi yote yaliyokuwa yamejitenga nayo.

Ingawa kuna uwezekano kuwa hatua hiyo ilichangiwa na uchaguzi unaokaribia, hali hiyo inahusishwa na tofauti za kisiasa na kikabila ambazo zimekuwepo baina ya viongozi

...Endelea Uk 26

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Makamu wa Rais Machar atimuliwa

Kutoka Uk 25

wakuu wa SPLM tangu nchi hiyo ilipopata uhuru. Licha ya viongozi wa SPLM kuonekana pamoja chini ya uongozi wa marehemu John Garang' wakati wa harakati za kujitenga na Sudan, kulikuwa na tofauti kali baina ya viongozi wakuu chamani. Tofauti hizo pia zilichangiwa na migawanyiko ya kikabila baina ya watu wa jamii ya Dinka, walio wengi zaidi nchini humo, na wa jamii ya Nuer, walio wa pili kwa wingi. Garang na Salva Kiir wanatoka jamii ya Wadinka huku Machar akitoka jamii ya Nuer.

Mnamo 1991, uhasama huo ulimfanya Machar na makamanda wengine kuunda chama pinzani kukabili walichotaja kuwa udikteta na ukosefu wa uwajibikaji katika SPLM.

Wakati mmoja, Machar alifanya kazi kwa karibu na serikali ya Sudan baada ya kutia saini mkataba wa amani na Rais Omar el-Bashir, aliyemfanya makamu wake. Ingawa baadaye alirudi SPLM na kuteuliwa makamu rais, Wadinka bado hawakumwamini. Hata hivyo, iliwalazimu kumvumilia ili kudumisha amani.

Kupatikana kwa uhuru kulifungua ukurasa mpya wa mzozo wa mamlaka baina ya viongozi wake. Kufuatia kifo cha Garang', aliyekuwa nguzo kuu katika kuunganisha SPLM, uhasama wa kisiasa na kikabila ulianza kuwatenganisha hata zaidi Machar na Kiir.

Rais Kiir alianza kuimarisha nguvu zake za kisiasa dhidi ya Machar, ambaye amekuwa akimuona kuwa tishio kwa ushawishi wake Sudan Kusini. Machar alipoanza kuonyesha dalili za kumkabili katika uchaguzi wa urais uliopangwa 2015, alimfuta kazi kama makamu wa rais. Pia aliwafuta kazi washirika wote wa Machar katika Baraza la Mawaziri.

Kiir alisema alichukua hatua hiyo baada ya kugundua baadhi ya washindani wake wa kisiasa walipanga kufufua migawanyiko katika SPLM. Huku akiungwa mkono na watu maarufu Sudan Kusini, Machar alifanya kikao na wanahabari Disemba 6, 2013, ambapo alimlaumu Machar kwa kuwa kiongozi dikteta.

Miongoni mwa waliomuunga mkono ni mjane wa Garang na mwanawe. Machar alionya kuwa "utawala wa mtu mmoja" ulikuwa hatari kwa umoja wa Sudan Kusini, huku akiapa hadharani kumkabili Kiir katika uchaguzi.

Katika nchi ambako vyama vya kisiasa na vikosi vya usalama huwa kitu kimoja, taharuki ilitanda miongoni mwa jeshi huku makamanda wakuu wakichukua misimamo ya kisiasa. Mapigano hayo yalisambaa haraka.

Asubuhi mapema Disemba 16, 2013, vikosi vilivyokuwa vikimuunga mkono Machar viliendesha operesheni kali jijini Juba, ambapo nusura vimng'oe mamlakani Rais Kiir. Ilimlazimu rais huyo kutafuta usaidizi wa kijeshi kutoka kwa Rais Museveni, aliyetuma wanajeshi na helikopta za kijeshi kumsaidia.



Waasi wa Sudan People's Liberation Movement-in-Opposition (SPLM-IO), kundi linalopinga serikali ya Sudan Kusini, wakilinda doria katika ngome yao mnamo Septemba 22, 2018, eneo la Panyume, Sudan Kusini, karibu na mpaka wake na Uganda.

Kwa upande wake, Machar alikuwa amepata usaidizi kutoka kwa Omar el-Bashir. "Uganda na Sudan zilichukua pande tofauti za kisiasa. Uganda ilitoa wanajeshi kumuunga mkono Salva Kiir na serikali ya Sudan Kusini, huku Sudan ikitoa usaidizi mdogo wa kijeshi kwa Machar na chama chake," akasema Ashley Quarcoo, ambaye ni msomi katika Kituo cha Kimataifa cha Kutetea Amani cha Canergie.

Uhasama kati ya mataifa hayo mawili umekuwa ukidhihirika kwenye mzozo wa Sudan Kusini. Kwa muda mrefu, Museveni alisaidia vikosi vya SPLM vilivyokuwa vikipigania uhuru wa Sudan Kusini kutoka kwa Sudan.

Kama hatua ya kulipiza kisasi, Rais Bashir alisaidia makundi ya wanamgambo ya Uganda, likiwemo kundi la Lord's Resistance Army (LRA), lililokuwa likijaribu kupindua serikali ya Museveni.

Uhasama huu ulionekana kumalizika baada ya Bashir kutimuliwa mamlakani kutokana na maasi makali ya raia. Kufuatia changamoto za kiuchumi zilizotokea kutokana na mapinduzi hayo, Sudan imekuwa ikijaribu kubuni ushirikiano wa kiuchumi na Sudan Kusini, hasa sekta ya kawi.

Chini ya mikataba hiyo, walisaidia kuleta maelewano pamoja na wanachama wengine wa IGAD, ambapo Machar na Kiir walikubali kuunganisha vikosi vyao kuwa chini ya uongozi mmoja. Hilo lilifikiwa baadaye Agosti, vikosi vyote vilipoingizwa katika Jeshi la Sudan, hali iliyoinuia matumaini ya amani ya kudumu. Hilo lilikuwa kimoja cha vikwazo vilivyokuwepo katika utekelezaji wa mkataba uliokuwa umetiwa saini na viongozi hao wawili.

Chini ya makubaliano yaliyotiwa saini 2020, ambayo matokeo yake yalikuwa kubuniwa kwa serikali ya mpito iliyoongozwa na Kiir na Machar, uchaguzi mkuu ulipangiwa kufanywa Desemba 2022. Hata hivyo, uchaguzi huo uliahirishwa hadi 2024 kutokana na makubaliano yaliyofikiwa kati ya pande hizo mbili.

Jamii ya kimataifa, hata hivyo, imeeleza shaka yake kuhusu kuahirishwa kwa uchaguzi huo, ikisisitiza kuwa lazima taratibu za kurudisha amani nchini humo zizingatiwe. Isitoshe, kutokana na mzozo unaoendelea katika SPLM na uchaguzi unaokaribia, baadhi ya wadadisi wanasema kuondolewa kwa Machar ni sehemu ya njama ya kupunguza umaarufu wake miongoni mwa wapigakura.

SPLM kinachukuliwa kuwa chama cha ukombozi ambapo yeyote atakayewania kwa tiketi yake atachaguliwa. Machar alikuwa katika nafasi ya kuchukua uongozi wa chama kutoka kwa Kiir kama angeamua kutogombes urais kutokana na hali yake mbaya kiafya. Lakini baada ya kutimuliwa, huenda ikawa vigumu kwa Machar kutumia rangi na nembo za chama, hali inayompa nafasi kubwa Kiir, au atakayemteua kama mrithi wake.

Kulingana na Profesa Kuol Nyuom kutoka Chuo Kikuu cha Juba, mabishano hayo yataongezeka jinsi uchaguzi unapokaribia.

*opiyo.levin@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya dunia

■ VITA VYA BUNGE: REPUBLICAN WAONGOZA KURA ZA MAONI

# AMERIKA YAAMUA 2022



Aliyekuwa Rais wa Amerika Barack Obama akisalimiana kwa mikono na wafuasi wake baada ya kuhutubia mkutano wa kampeni kuunga mkono wanachama wa Democrats wa jimbo la Nevada katika Shule ya Upili ya Cheyenne, Novemba 1, Kaskazini mwa Las Vegas.

*Wingi wa Democrats katika Bunge ni mwembamba sana: Seneti imegawanyika 50-50 (Kura ya Makamu Rais Kamala Harris ikileta tofauti na kuwafaidi) na Spika Nancy Pelosi akiwa anaongoza Bunge kunawapa wingi mwembamba sana. Viti vyote 435 vya Bunge na 35 kati ya 100 vya Seneti vinashindaniwa debeni. Aidha, magavana 36 kati ya 50 wa majimbo wanachaguliwa*

● WASHINGTON

Amerika inafanya uchaguzi wa kati ya muhula Novemba 8. Matokeo yatakuwa na athari kubwa kwa miaka miwili inayobakia ya urais wa Joe Biden na baadaye. Shauku ya chama cha ya kutawala na malalamishi yake kuhusu hali ya uchumi yanakiweka katika hali nzuri ya kudhibiti Bunge la Wawakilishi la Amerika, kulingana na utafiti wa CNN uliofanywa na SSRS.

Utafiti huo unaonyesha kuwa hamu ya wafuasi wa chama cha Democratic ya kupiga kura iko chini sana kuliko ilivyokuwa 2018, chama hicho kilipodhibiti Bunge.

Wapigakura wa Republican katika kura mpya ya maoni wanafuatilia sana uchaguzi wa kati ya muhula wa mwaka huu kuliko wale wa Democratic katika maswali kadhaa ya kutathmini matokeo ya uchaguzi.

Kwa jumula, asilimia 27 ya wapigakura waliosajiliwa wanasema wana hamu sana ya kupiga kura mwaka huu, ikiwa imepungua kutoka asilimia 37 kabla ya uchaguzi wa kati ya muhula wa 2018, ilhali kuna kushuka kwa hamu ya kupiga kura miongoni mwa wanachama wa Democratric.

Miaka minne iliyopita, asilimia 44 ya wapigakura wa Democratic walisema walikuwa na hamu kubwa ya kupiga kura; sasa ni asilimia 24 wanaosema hivyo. Miongoni mwa wanachama wa Republican, idadi imepungua kidogo, kutoka asilimia 43 hadi asilimia 38.

Ingawa kwa jumla hamu ya kupiga kura sasa iko chini kuliko ilivyokuwa Oktoba 2010, hamu kubwa ya wanachama wa Republican sasa, ni sawa na pengo lililoibuka katika kura ya

Endelea Uk 28

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Ushindani mkali kudhibiti Bunge la Amerika

Kutoka Uk 27

maoni ya CNN wakati huo, kabla ya matokeo mazuri ya chama hicho katika uchaguzi wa kati ya muhula.

Wakati huo, ilivyo wakati huu, chama cha Republican kilikuwa mbele kwa alama 14, maana kuwa walikuwa na hamu ya kupiga kura katika uchaguzi wa kati ya muhula (asilimia 31 ya wapigakura wa Republican walikuwa na hamu kubwa ikilinganishwa na asilimia 17 ya wapigakura wa Democratic).

Katika kura hiyo ya maoni, chama cha Republican kinaongoza Democrat katika swali kwa wapigakura kuhusu mgombeaji wanayemtaka katika wilaya zao kwa asilimia 51 dhidi ya asilimia 47 miongoni mwa wanaosema watapiga kura, uongozi mwembamba sana.

Miongoni mwa wapigakura waliosajiliwa, vyama vyote vinatoshana nguvu, huku asilimia 47 wakiunga Republican na asilimia 46 wakiunga Democratic. Hali kama hii inapotokea, Republican hushinda viti vingi Bungeni.

Hali ya Republican katika vita vya kudhibiti Bunge mwaka huu inapigwa jeki na malalamishi kuhusu hali ya uchumi wa nchi hiyo.

Uchumi na mfumko wa bei ni masuala muhimu yanayohusu wapigakura katika mkondo huu wa mwisho, huku karibu nusu ya wanaosema watapiga kura (asilimia 51) wakisema hayo yatakuwa masuala muhimu yatakayoamua watakavyopiga kura za ubunge.

Wapigakura wa Democratic wamegawanyika zaidi, huku uchumi na uavyaji mimba yakiwa masuala yanayoongoza kwa karibu asilimia sawa – 29 kwa uavyaji mimba, asilimia 27 kwa uchumi na mfumko wa bei.

Wanaosema uchumi ndilo suala kuu kwao ni wengi katika ngome za Republican, ikiwa ni asilimia 71 hadi 26. Kwa tofauti kubwa zaidi, wanasema wanaamini chama cha Republican hasa kinaweza kushughulikia vyema zaidi uchumi na mfumko wa bei (asilimia 71 Republican dhidi ya asilimia 18 ya Democratic).


Kura hiyo ya maoni iligundua mtazamo unaopanuka kuwa tayari uchumi umedorora, huku watu wengi zaidi pia wakisema kwa jumla hali katika nchi inaendelea kuwa mbaya.

### Uchaguzi wa kati ya muhula ni nini na ni nani anachaguliwa?

Huu ni uchaguzi wa ubunge, ambao una sehemu mbili - Bunge la Wawakilishi na Seneti.

Uchaguzi huu unafanywa baada ya miaka miwili na huwa katikati ya muhula wa miaka minne wa rais aliye mamlakani, unaitwa uchaguzi wa kati ya muhula.

Bunge la Congress hutunga sheria zinazotumiwa nchini. Linaamua sheria za kupitishwa na Seneti inaweza kuzikataa au kuziidhinisha, kuidhinisha uteuzi unaofanywa na rais, na nadra sana, kumchunguza rais. Kila jimbo lina maseneta wawili, wanaohudumu kwa miaka sita. Wawakilishi wanahudumu miaka miwili na wanawakilisha wilaya ndogo.



Rais wa Amerika Joe Biden amkumbatia mgombeaji wa kiti cha Seneti, Rep Val Demings (D-Florida) huku mgombeaji wa ugavana Charlie Crist akiangaliia wakati wa mkutano katika Chuo Kikuu Florida Memorial, mnamo Novemba 1.

### Nani anaweza kushinda?

Chama cha Democratic kimekuwa na idadi kubwa katika mabunge yote mawili kwa miaka miwili iliyopita. Hilo limemsaidia Rais Joe Biden kupitisha sheria alizotaka. Lakini wingi wa chama cha Democratic ni mwembamba sana dhidi ya Republican, jambo linalofanya uchaguzi unaokuja kuwa na ushindani mkali.

Kura za maoni zinaonyesha kuwa huenda Republican kikashinda viti vingi katika Bunge lakini Democratic kinaweza kuwa na vingi katika seneti. Kati ya viti 435 vya Bunge, vingi vinashikiliwa na vyama hivyo viwili na ni 30 vinavyong'ang'aniwa na vyama hivyo.

Maeneo yaliyo karibu na miji katika majimbo kama Pennsylvania, California, Ohio na North Carolina yatakuwa muhimu.

Katika seneti, sasa inaonekana kuwa vinne kati ya viti 35 vinavyoshindaniwa vinaweza kuendea kimoja cha vyama hivyo viwili. Ushindani mkali hapa uko Nevada, Arizona, Georgia na Pennsylvania.

### Ni masuala gani makubwa?

Mwanzoni mwa 2020, ilionekana kama masuala makuu yalikuwa uhamiaji, uhalifu na gharama ya maisha, ambayo hushindia kura wanachama wahifadhina wa Republican.

Haya yalibadilika Juni Korti ya Upeo ilipobatilisha kinga dhidi ya uavyaji mimba, na kupiga jeki chama cha Democratic, kinachounga mkono wanawake kuwa na haki ya kuamua. Lakini athari za uamuzi huo zinapofifia, chama cha Republican kinajaribu kurudisha kampeni katika masuala ya mfumko wa bei, uhamiaji na uhalifu wa kutumia nguvu.

### Matokeo yatakuwa na athari gani?

Uchaguzi wa kati ya muhula huwa kama uamuzi kuhusu utendakazi wa rais na chama kinachotawala huwa kinapoteza viti. Huo ndio wasiwasi wa Rais Biden, ambaye umaarufu wake miongoni mwa wapigakura umekuwa chini ya asilimia 50 tangu Agosti mwaka huu.

Kama Democratic kitadumisha wingi wake, Rais Biden ataweza kuendelea na mipango yake kuhusu mabadiliko ya tabia nchi, kupanua mipango ya huduma za afya ya serikali, kulinda haki za uavyaji mimba na kukaza sheria za kumiliki bunduki.

Chama cha Republican kikitwaa moja la mabunge kitaweza kukwamisha ajenda ya Biden. Pia kitaweza kudhibiti kamati za uchunguzi, na kinaweza kuzima uchunguzi wa shambulizi la Januari 6 katika majengo ya bunge la Amerika na wafuasi wa aliyekuwa Rais Donald Trump - ingawa unatarajiwa kukamilika kufikia mwisho wa mwaka huu.

Kinaweza pia kuanza uchunguzi mpya katika masuala kinayofuatilia kama vile uhusiano wa kibiashara ya mwanawe Biden na China, au kuondolewa kwa wanajeshi wa Amerika Afghanistan. Itakuwa vigumu kwa Biden kufanya uteuzi mpya, ikiwemo katika Mahakama ya Upeo ya Amerika.

Republican kikidhibiti mabunge kinaweza pia kulemaza sera ya kigeni - hasa usaidizi kwa Ukraine, inayopigana na uvamizi wa Urusi. Rais Biden anaweza kutumia mamlaka yake kukataa sheria za wahifadhina kuhusu uavyaji mimba, uhamiaji na ushuru. Matokeo? Kukwama hadi uchaguzi ujao wa urais na ubunge.

### Hii itaathiri vipi kampeni za urais 2024?

Uchaguzi wa kati ya muhula utatoa vidokezo kuhusu anayeweza kuwa mgombeaji wa urais wa chama cha Republican katika uchaguzi wa 2024. Kama wagombeaji wanaoungwa mkono na Bw Trump watashindwa, huenda asiungwe mkono na chama cha Republican kuwania urais tena. Katika majimbo ya Florida na Texas, magavana wa Republican Ron DeSantis na Greg Abbott wana matumaini ya kuchaguliwa tena ili kuinua azma yao ya kuingia Ikulu.

Kama Democratic watashikilia mamlaka Michigan, Wisconsin na Pennsylvania, hilo litawapa imani wanapojiandaa kwa kampeni zao za 2024 kufanya Rais Biden kuchaguliwa tena.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "ePaper Copy"

kurunzi ya dunia

KUANZIA CHURCHILL HADI LULA, WANATUMIA MBINU GANI?

# SIRI YA KURUDI MAMLAKANI

*Kurrudi kwa Lula kutoka nyika ya kisiasa hadi katika urais kwawapa motisha viongozi wengi duniani*



Benjamin Netanyahu

Jacob Zuma

Donald Trump

● RIO DE JANEIRO

Huku Luiz Inacio Lula da Silva wa Brazil akisherehekea kurejea kutoka jela na kuanza awamu ya tatu akiwa rais, tunatazama viongozi wengine waliorejea kutoka kwenye nyika ya kisiasa – na wanaotumai kuiga mfano wao.

Mwanasiasa huyo aliyeweka viwango bora zaidi vya uongozi nyakati za vita aliteleza vibaya katika Vita vya Kwanza vya Dunia, aliposababisha mauaji ya maelfu ya vikosi vilivyoshirikiana naye katika vita hivyo eneo la Gallipoli.

Churchill alijiuzulu kama waziri wa jeshi la majini kwa fedheha tele, lakini akarudi kuongoza Uingereza kwa ushindi dhidi ya jeshi la Nazi la Ujerumani katika Vita vya Pili vya Dunia, huku akipatia taifa mshawasha kwa hotuba za aina yake.

Mnamo Julai 1945, chama cha Conservative kilitupwa nje lakini Churchill akakirudisha mamlakani tena baadaye 1951 akiwa na umri wa miaka 76.

Kiongozi wa Uasi nchini Ufaransa katika Vita vya Pili vya Dunia alikuwa shujaa katika Ukombozi wa Ufaransa mnamo Agosti 1944. Lakini baada ya miaka miwili tu alijiuzulu kama kiongozi wa serikali ya mpito Ufaransa baada ya kukosa kuungwa mkono kutimiza ndoto yake ya kuwa na mtindo thabiti wa urais sawa na Amerika.

Aliitwa tena mnamo 1958 kuongoza nchi wakati wa vita vya kupigania uhuru wa Algeria kutoka kwa Ufaransa na akatumia fursa hiyo kushinikiza katiba mpya iliyompa rais mamlaka zaidi.

Rais wa Argentina kuanzia 1946 hadi 1955 pamoja na mke wake, Eva, waliasisi vuguvugu la haki ya kijamii kwa jina "Peronism" ambalo bado linaheshimiwa sana katika mrengo wa kushoto nchini Argentina na kuwa chukizo kwa mrengo wa kulia.

Lakini aling'olewa mamlakani kupitia mapinduzi ya serikali na akatorokea nchini Paraguay, kisha Madrid, kabla ya kurudi Argentina kwa shangwe na vifijo mnamo 1973. Alihudumu kwa awamu nyingine ya miezi tisa kama rais kabla ya kifo chake.

Deng Xiaoping, kiongozi mwenye nguvu zaidi China kutoka mwishoni mwa miaka ya 1970 hadi kifo chake mnamo 1997, alibanduliwa mara mbili wakati wa Mageuzi ya Kitamaduni. Alifurushwa nchini humo na kiongozi wa mageuzi Mao Zedong mnamo 1966 akitajwa kuwa "chombo cha ubepari." Alikuwa akifanya kazi katika kiwanda cha kutengeneza trekta.

Alirudishwa mnamo 1973, akaondolewa tena 1976 na waasi waliomunga mkono Mao "Gang of Four", lakini akarudi kama kiongozi halisi baada ya kifo cha Mao baadaye mwaka huo ambapo aliongoza mabadiliko ya China kuwa taifa lenye uwezo mkubwa wa kiuchumi ulimwenguni.

Kiongozi wa kutetea demokrasia Myanmar alishinda uchaguzi mnamo 1990 lakini jeshi la serikali iliyokuwa ikitawala wakati huo ikakataa kumkabidhi mamlaka.

Alitumia sehemu kubwa ya miongo miwili iliyofuata katika kifungo cha nyumbani kabla ya kuwa waziri mkuu mnamo 2016 kufuatia ushindi wa chama chake katika uchaguzi huru wa kwanza katika robo ya karne.

Lakini uhuru wake ulikuwa wa muda mfupi sana. Jeshi lilitimua serikali yake kwa mara nyingine mnamo Februari 2021 na tangu hapo limemhukumu kifungo cha jumla ya miaka 26 gerezani.

Aliyekuwa waziri mkuu mara tatu wa Italia, Silvio Berlusconi, amerudi mara nyingi sana kiasi kwamba amepachikwa jina la utani kama "asiyekufa".

Bilionea huyo mwenye umri wa miaka 86 alifanya hivyo tena katika uchaguzi wa taifa hilo uliofanywa Septemba 25, akarudi Seneti, miaka tisa baada ya kurushwa nje kwa sababu ya udanganyifu kuhusu malipo ya ushuru.

Berlusconi, aliyeendesha kampeni kama babu mkarimu, pia alinusurika kashfa nyingine inayohusu karamu za kula uroda alizoandaa akiwa waziri mkuu. Chama chake kiko kwenye muungano na Waziri Mkuu anayeegemea mrengo wa kulia Giorgia Meloni.



Mgombeaji wa Workers Party, Luiz Inacio Lula da Silva, akiwasalimu wafuasi wake katika ukumbi wa Paulista, jijini Sao Paulo, Brazil, baada ya kushinda urais mnamo Oktoba 30.

**Donald Trump**

Mmoja wa marais waliosababisha migawanyiko mingi zaidi katika historia ya Amerika amedokeza huenda akagombea tena 2024 huku akiendelelea kutoa madai ya uongo kuwa ndiye aliyeshinda uchaguzi uliopita.

**Benjamin Netanyahu**

Waziri mkuu wa Israel aliyehudumu kwa muda mrefu zaidi, ambaye alitimuliwa mnamo Juni 2021, anatumai kunyakua tena wadhifa huo mkubwa baadaye Novemba 1, licha ya kushtakiwa kwa ufisadi.

**Jacob Zuma**

Aliyekuwa rais wa Afrika Kusini mwenye umri wa miaka 80 aliyelazimika kujiuzulu mnamo 2018 kuhusiana na madai ya ufisadi, anataka kurudi mamlakani Disemba, chama tawala cha African National Congress kitakapofanya chaguzi za uongozi.

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

Nation Media Group "ePaper Copy"

## TANZIA

■ ALITAMBULIWA KWA KUMUINGIZA UHURU KATIKA SIASA ZA GATUNDU

# DALALI WA KISIASA ALIYESITASITA

*Ingawa hajulikani sana nje ya siasa za Kiambu, David Kigochi alichangia sana Uhuru Kenyatta kuingia katika siasa*

• NA JOHN KAMAU

Kama David Kigochi, aliyefariki wiki hii, hakumualika Uhuru Kenyatta katika Kundi la Wataalamu kutoka Gatundu, pengine rais huyo mstaafu hangeingia katika siasa wakati huo.

Uhuru, wakati huo akiwa na miaka 34, alikuwa ametosheka na kiwango alichokuwa amefikia maishani. Wakati huo, alikuwa mwembamba na mpenda raha, na alionyesha taswira ya mfanyabiashara ambaye hakuwa amepiga hatua sana kifedha.

Alikuwa akifuga nywele yake kwa mtindo wa Afro. Alikuwa mvuta sigara, mwenye wasiwasi na asiyezingatia usafi.

Kigochi alihofia kuwa Bw Kenyatta - ambaye alikuwa amemjua kwa miaka mingi - alikuwa akijipoteza kimaisha. "Ilibidi tumuingize katika siasa," akaniambia Kigochi, kwenye mmoja wa mikutano mingi tuliyofanya katika afisi yake ya kibinafsi, karibu na bustani ya Jevanjee. "Nilienda nikazungumza na mama yake."

Kigochi amekuwa akidai ndiye alimuingiza Uhuru katika siasa za Gatundu. Ajabu ni kuwa hakujiunga na madalali wa kisiasa waliomzunguka Uhuru. "Akinihitaji, ana namba yangu ya simu," angesema.

Alipenda kukaa hadi nyakati za usiku katika afisi yake - na alikuwa msimuliaji stadi wa matukio. Kwa mwanahabari, alikuwa kitovu cha habari. Simulizi zake zilihusu hadhi yake. "Uhuru angeketi mahali ulipoketi na kunywa mvinyo - au kwenda kununua kuku katika ghorofa za chini."

Kigochi alipenda mvinyo maalumu - hali iliyoonekana kuchangiwa na kazi yake katika Wizara ya Utalii, ambako alihudumu kama Mkaguzi wa Hoteli kadhaa.

Kama mtumishi wa umma, Kigochi hangeshiriki siasa. Kinaya ni kuwa, alifanya hivyo kwa furaha. Alikuwa na ushirika mzuri wa mawakala wa kisiasa katika Mkoa wa Kati kama vile Katibu Mkuu wa Kanu, Joseph Kamotho na makatibu wakuu Chrispus Mutitu na Wamatu Njoroge. Angeonekana kwenye baadhi ya mikutano yao ya Harambee, ambako masuala ya siasa na mamlaka yaliendeshwa bila mipaka. Kama mwenyekiti wa Wataalamu kutoka Gatundu, Kigochi aliongoza eneobunge lililompa nafasi muhimu sana katika siasa za nchi.

Baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya kisiasa nchini mnamo 1991, Kigochi alikuwa miongoni mwa watu wachache wa jamii ya Kikuyu waliounga mkono utawala wa Kanu. Rais wa zamani, Daniel Moi, alipoanza kushawishi eneo la Mlima Kenya kurudi katika Kanu, Kigochi alikuwa mmoja wa wanachama wa Kundi la Kusimamia Maendeleo katika Mkoa wa Kati. Kundi hilo lilijumuisha wasimamizi wa mashirika ya serikali na wafanyabiashara kutoka Mlima Kenya.

Kigochi na Njoroge walitaka kumuingiza jamaa wa familia ya Kenyatta katika Kanu. Wakati huo, familia hiyo haikuwa na mrithi yeyote katika siasa, na jamaa zao wa mbali walikuwa katika Upinzani.

Baada ya kifo cha Mzee Kenyatta mnamo 1978, mwanawe mkubwa, Peter Muigai, wakati huo akiwa Mbunge wa Juja, pia alifariki mnamo 1979. Mwanawe mkubwa wa kike, Margaret Kenyatta, alitosheka na wadhifa wa ubalozi, baada ya kushindwa kwenye chaguzi jijini Nairobi.

Kiti cha ubunge cha Gatundu, ambacho kilikuwa kimeshikiliwa na Jomo, kilichukuliwa na mpwa wake, Ngengi Muigai. Nduguye Mama Ngina Kenyatta, George Muhoho, alishinda ubunge katika eneo la Jula, ingawa alikuwa katika chama cha Democratic Party (DP) cha Mwai Kibaki.

Mnamo Agosti, 1995, Wataalamu kutoka Gatundu walijitayarisha kumpeleka Uhuru kukutana na Rais Moi ili kupata baraka zake. Akiwa na umri wa miaka 34 pekee, ilikuwa mara yake ya kwanza kuongoza ujumbe kama huo, huku ajenda kuu zikiwa kahawa na siasa.

Wakati huo, tawi dogo la Kanu Gatundu lilikuwa likiongozwa na Bw Patrick Muiruri, aliyefanya kila awezalo kuokoa Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Kahawa cha Gatukuyu dhidi ya kuvurugwa na siasa za eneo hilo. Wakati wa mkutano huo katika Ikulu, na kama ilivyokuwa imepangwa na kundi la Kigochi, Moi alivunja uongozi wa Kanu katika eneo hilo ili kumtengenezea njia Uhuru kuingia katika siasa.



David Kigochi

Alivunja pia Chama cha Ushirika cha Gatukuyu, ambacho Muiruri alikuwa ameongoza hadi 1985, wakati kilivunjwa katika vyama 12 vya ushirika.

Hilo ndilo lilitumiwa kumuingiza Uhuru katika siasa za Gatundu. Ingawa Gatundu ilikuwa na vyama vingine vinne vya ushirika - Kanyoni, Gatundu, Gathage na Kamwangi - ni Gatukuyu pekee kilichovunjwa.

Mwezi uliotangulia, mchango wa Kigochi katika 'kifo' cha Gatukuyu uliibuka, baada ya kuhudumu kama mwangalizi akiwa na Uhuru kwenye uchaguzi wa chama hicho. Kundi la Muiruri lilitaja uchaguzi huo kutofaulu, likidai ulisusiwa na wanachama.

Ingawa Amos Gatoto alichaguliwa mwenyekiti, Ikulu iliagiza chama kivunjwe. Mzozo uliibuka baadaye ilipobainika chama hakikuwa kimelipwa Sh13 milioni kutokana na mauzo ya kahawa.

Kupanda kwa Uhuru katika siasa za Kiambu pia kulimkweza Kigochi kisiasa. Mnamo 1997, Kundi la Maendeleo ya Mkoa wa Kati lilimfadhili Kigochi kuwania ubunge Gatundu Kaskazini, huku Uhuru akigombea Gatundu Kusini. Iliamini kuwa ndiye alifaa kuwakabili Patrick Muiruri, ambaye alikuwa amejiunga na Social Democratic Party (SDP) cha Charity Ngilu, na bwanyenye Clement Gachanja kutoka Kiambu, aliyehudum kama mbunge wa Dagoretti. Hata hivyo, hakushiriki katika uchaguzi huo. Badala yake, alibuni na kusajili chama chake, Farmers' Party (FP), kinachoongozwa na Irungu Nyakera.

Kigochi alionekana hadharani mara ya mwisho Machi, chama chake kilipokuwa kikiungana na mrengo wa Kenya Kwanza. Ingawa hajulikani sana nje ya siasa za Gatundu, mchango wake katika safari ya mwanzo ya kisiasa ya Uhuru Kenyatta unajulikana sana. Pengine, Kigochi ni dalali wa kisiasa aliyesitasita.

***jkamau@ke.nationmedia.com***
***@johnkamau1***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep





**SMS the word GAZETI to 20567,**
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE SMS text and FREE Delivery**

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*


SPORT ON!
JAMES
WOKABI
BERNARD
NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM